# Nipashe

Jumatatu Januari 16, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581192

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710 LIKE & FOLLOW US









**Wadaiwa** kuua wake zao kisa wivu, mmoja anywa sumu baada ya kuua

UK. 8





UKURASA 11

RIPOTI MAALUM

# Watoto wafundishwa kulawitiana shuleni




• **Wahusika** wakuu watajwa, butwaa mkoani hadi wizarani... *Uk. 4*



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akipewa maelezo na mshiriki wa mashindano ya 'global robotic challange' Maria Mtega, kuhusu roboti iliyoundwa na vijana wa Kitanzania ya kukamata hewa ukaa (Carbon dioxide), jijini Dar es Salaam jana. Mashindano hayo yalifanyika nchini Geneva, Uswisi na kujumuisha zaidi ya mataifa 190. Katikati ni Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye. **Habari kamili Ukurasa 2. PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU.**

## YALIYOMO

UKURASA WA 5

### MWALIMU WA MADRASA MBARONI TUHUMA KUNAJISI WANAFUNZI

MWALIMU wa madrasa kwenye Msikiti wa Kebeyo, Kijiji cha Getenga, Tarafa ya Inchugu wilayani Tarime mkoani Mara, Shaban Harun (37) anashikiliwa na Jeshi la Polisi Kituo cha Sirari kwa tuhuma za kuwanajisi wanafunzi wake wawili wenye...

UKURASA WA 18

### 'MARUFUKU WALIMU KUPIGAPICHA WANAFUNZI KURUSHA MITANDAONI'

MKUU wa Wilaya ya Mkalama, Sophia Kizigo, amewaonya walimu wilayani humo kutumia vishikwambi walivyokabidhiwa na serikali kwa...

# CHADEMA kuanza na hoja 10 mikutano ya hadhara

UKURASA 2

# Nauli mpya DART kuanza rasmi leo

UKURASA. 5

**MICHEZO** **KAMPENI UCHAGUZI SIMBA ZAANZA** UK.20

**MAONI, KATUNI** UK.6



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Adolf Mkenda (katikati) akiwa na wanafunzi wenye ulemavu wa Shule Maalumu ya Lukuledi Masasi mkoani Mtwara jana wakati wa uzinduzi wa shule hiyo jana **PICHA: HAMISI NASRI.**

# CHADEMA kuanza na hoja 10 mikutano ya hadhara

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kinatarajia kuzindua ajenda zaidi ya 10 zitakazokiongoza kwenye mikutano yake ya hadhara ambayo itazinduliwa jijini Mwanza Januari 21 mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari mkoani Dar es Salaam jana kuhusu uzinduzi wa ajenda hizo, Mkurugenzi wa Itikadi, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa chama hicho, John Mrema alisema utakwenda sambamba na uzinduzi wa mikutano ya hadhara kwenye kanda mbili ambazo ni Kanda ya Ziwa Viktoria na Serengeti mkoani Mara.

Pasina kuzitaja ajenda hizo, Mrema alisema mchakato wake utaongozwa na Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Freeman Mbowe na viongozi wengine wa kitaifa.

Mrema alisema: "Hadi sasa maandalizi yanaendelea kwa kutoa taarifa kwenye vyombo husika hususani Jeshi la Polisi na kuomba viwanja kwenye halmashauri husika. Hatutegemei kwamba kutakuwa na figisu za aina yoyote katika hili".

Alisema wamelazimika kuzindua mikutano ya hadhara Januari 21 mwaka huu kwa sababu wanaadhimisha pia miaka 30 tangu chama hicho kilipopata usajili wa kudumu Januari 21, 1993.

"Kwetu hii ni siku kubwa kwa sababu ndiyo siku ambayo chama chetu kilipata usajili wa kudumu. Baada ya miaka saba ya kutoruhusiwa kufanya mikutano ya hadhara, tumeona tuanze kwenye siku hii muhimu katika historia ya chama chetu," alisema.

Mrema alisema Kamati Kuu ya CHADEMA ilifanya kikao Januari 5 mwaka huu kwa njia ya mtandao na kuazimia uzinduzi wa mikutano ya hadhara ufanyike siku hiyo.

"Kwa hiyo, kuna mambo ambayo tutakwenda kuyasema, ndiyo yatakayotuongoza katika mikutano yetu ya hadhara na baada ya uzinduzi, ngazi nyingine zitaendelea. Pamoja na ajenda za kitaifa, pia kuna ajenda za maeneo mahususi," alisema Mrema.

## MATUMIZI YA LUGHA

Kuhusu maelekezo ya kutumia lugha ya staha katika mikutano ya hadhara yaliyotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan wakati akitangaza rukhsa ya mikutano hiyo nchini, Mrema alisema watalenga kutoa hoja na siyo lugha chafu.

"Mtu anapotoa lugha za matusi, za kashfa, za kutweza, kwenye mikutano ya hadhara, nchi yetu siyo maskini wa sheria, zipo sheria zinazosimamia hotuba.

"Sisi ni chama cha siasa chenye umri wa miaka 30, tuna sera, tuna ajenda zetu, hatuoni sababu ya serikali kuwa na hofu eti CHADEMA itaenda kutukana.

"Tuwahakikishie Watanzania tunakwenda kufanya mikutano ya hoja, tutatembea na hoja zaidi ya 10 ambazo tunakwenda kuzizindua kwa ajili ya kuwa rejea ya hotuba za viongozi wetu mbalimbali wanapofanya mikutano ya hadhara," alifafanua.

## MAPOKEZI YA LISSU

Mrema pia alizungumzia mapokezi ya Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA Tanzania Bara, Tundu Lissu, akisema kuwa maandalizi ya kumpokea kiongozi wao huyo yanaendelea.

Alisema maandalizi hayo yanakwenda sambamba na kuwapokea viongozi wengine wanaoishi nje ya nchi akiwamo Godbless Lema.

Mrema alisema: "Maandalizi ya mapokezi ya Tundu Lissu yanaendelea na tutatoa taarifa rasmi juu ya utaratibu, njia atakayopita na mapokezi yatakuwaje.

"Na kuhusu viongozi wengine wa chama chetu kurejea nchini, akiwamo Godbless Lema, tunaendelea kufanya na watakapokamilisha taratibu zao, watasema wanarejea lini.

"Lakini maandalizi yanaendelea huko waliko na yako hatua mbalimbali. Kwa hiyo, wakikamilisha tutatoa taarifa rasmi," alisema.

## SHERIA YA HABARI

Mrema pia aligusia marekebisho ya Sheria ya Huduma ya Vyombo vya Habari ya Mwaka 2016, akisema katika mazungumzo yanayoendelea kati yao, serikali na Chama Cha Mapinduzi (CCM), wanataka kufanyike marekebisho ya sheria hiyo.

"Kwenye mazungumzo yanayoendelea, kati ya sheria ambazo tunafikiri ni za awali za kufanyiwa marekebisho au kuandikwa upya ni pamoja na Sheria ya Huduma ya Vyombo vya Habari, kwa sababu huwezi kurudi kwenye mikutano ya hadhara kama umevifunga vyombo vya habari mikono nyuma, mikutano hiyo haitawafikia wananchi.

"Kwa hiyo, kwenye hii sheria pamoja na ile ya makosa ya kimtandao, tunatamani angalau zikafanyiwe marekebisho ikiwezekana katika Bunge la Februari mwaka huu ili vyombo vya habari viwe huru na vikafanye kazi yake bila hofu," Mrema aliwasilisha hoja yao.


**KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI**

**DIANA EMMANUEL MATIAS** anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 477 DDV** aina ya **KINGLION** yenye Chassis namba **LZL15P0902MHL45775.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **GEI/CHA/RB/13262/2023.**

2172229101



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya MASWA.**

**Kituo cha NYALIKUNGU mkoa wa SIMIYU**

**Shauri la Madai/Ndoa Na.62/2022**

**Jina la mdai: ELIZABETH JAMES**

**Jina la mdaiwa: EMMANUEL PHILBERT**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa:EMMANUEL PHILBERT**
**WA BIAFRA "B"**
**MASWA MJINI**

**K.K AFISA MTENDAJI**
**KATA YA SHANWA**
**MASWA.**

Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba (Eleza habari ya madai)Anadai talaka ili muachane hivyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 30 Mwezi 01 Mwaka 2023 saa 2:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila wewe kuwepo.

Imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 13 Mwezi 01 Mwaka 2023..

MAHAKAMA YA MWANZO NYALIKUNGU MASWA

HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO NYALIKUNGU

2172229201


# Samia apongeza Watanzania kupata medali ya ubunifu

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan amewapongeza vijana wa Kitanzania walioibuka washindi wa pili na kupata medali ya fedha katika mashindano ya kwanza ya Global Robotics Challenge yaliyofanyika Geneva, Uswisi na kushirikisha mataifa zaidi ya 190.

Amefarijika kusikia kuwa roboti iliyoundwa na vijana kutoka Tanzania chini ya maudhui ya kukamata hewa ukaa, inaweza kusaidia kusafisha kaboni hewani na kusaidia kupunguza ongezeko la joto kwenye angahewa ya dunia.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa kwa niaba ya Rais Samia katika hafla ya kuwapongeza vijana hao iliyofanyika kwenye Ukumbi wa Ofisi Ndogo ya Waziri Mkuu, Magogoni jijini Dar es Salaam.

Alisema hayo ni mafanikio makubwa na Watanzania wote wanapaswa kujivunia kwa kuiwakilisha nchi vizuri.

"Nitumie nafasi hii kuwaahidi kuwa serikali kupitia Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari itaendelea kufuatilia maendeleo yenu na kuona namna ya kuendeleza vipaji vyenu," alisema.

Waziri Mkuu alitumia fursa hiyo kuielekeza Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari iandae mpango wa kuwa na vituo vya ubunifu nchini katika ngazi za mikoa na wilaya mbalimbali ili kusaidia kuinua vipaji vya vijana.

Aliagiza wizara iimarishe utaratibu wa kuwatambua na kuwaendeleza wabunifu mbalimbali ili kuwapa motisha na kukuza ajira nchini na ishirikiane na mamlaka husika kuandaa utaratibu wa kuwasaidia wabunifu mbalimbali na kuwaunganisha na taasisi pamoja na kampuni kwa ajili ya kuendeleza ubunifu wa kazi zao kulingana na mahitaji.

Waziri Mkuu pia alielekeza wizara hiyo na mamlaka husika zijipange kuwekeza katika kulinda usalama wa taarifa za watumiaji wa mifumo mbalimbali ya TEHAMA sambamba na kutoa elimu kuhusu usalama sahihi wa vifaa na matumizi salama ya mifumo ya kompyuta.

Alielekeza wizara hiyo kupitia Tume ya TEHAMA ifanyie kazi vikwazo mbalimbali vya kisera na kikodi vinavyoleta changamoto kwa wabunifu katika masuala ya TEHAMA na matokeo ya ubunifu mbalimbali yawekewe utaratibu wa kufanywa kuwa bidhaa na kupata soko badala ya kuwekwa maktaba.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye aliipongeza Kampuni ya Mawasiliano ya Tigo kwa kuamua kutumia sehemu ya mapato yao kwa kuwasaidia vijana wa kike nchini katika kuendeleza ubunifu kupitia APPS and Girls.

Waziri huyo alisema takwimu mbalimbali zinaonyesha kuwa ushiriki wa mabinti na wanawake katika matumizi ya TEHAMA si mzuri sana, barani Afrika asilimia 24 tu ya wanawake wanashiriki kwenye TEHAMA huku wanaume ni asilimia 35.

"Tanzania ukienda shuleni, watu wanaosoma Computer Science na mambo yanayohusiana na TEHAMA, wanawake ni asilimia 10 tu, ni muhimu kuendelea kuongeza nguvu katika kupunguza pengo hilo," Nape alisema.

Ofisa Mkuu wa Udhibiti wa Kampuni ya MIC Tanzania PLC (TIGO), Innocent Rwetabula alisema kampuni yao inafanya kazi kwa kuzingatia vipaumbele vya serikali kwa sekta ya mawasiliano na kuongoza safari ya kidigitali hadi kufikia Tanzania ya kidigitali.

Alisema lengo la ufadhili huo ni kuziba pengo kati ya wavulana na wasichana katika sayansi, teknolojia, uhandisi na hisabati (STEM), kutoa ujuzi na stadi za ujasiriamali kupitia utoaji wa mafunzo ya TEHAMA, ushauri na uanzishaji wa biashara mpya za kiteknolojia ambapo mwaka jana wasichana 1,590 walinufaika na mpango huo.

Akizungumzia kuhusu shindano la kwanza la Global Robotics Challenge, ofisa huyo alisema hufanyika kila mwaka kwa mtindo wa Olimpiki na kaulimbiu ya mwaka huu ilikuwa ni cabon capture, ambayo ni mchakato wa kukamata hewa ukaa iliyopo na kuzuia isiingie angani. Kundi la wanafunzi watano kati ya 11 waliiwakilisha nchi na kupata nafasi ya pili.

## HABARI KITAIFA

# Ukuaji deni la ndani tishio maendeleo ya wananchi - ACT



**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha ACT Wazalendo kimesema ukuaji wa deni la ndani kwa Taifa unatishia ustawi wa maendeleo ya wananchi, kikiitaka serikali kuchukua hatua za haraka kukabiliana na ongezeko hilo.

Kimesema mwenendo huo wa kukua kwa deni la ndani umesababisha athari mbalimbali ikiwamo nchi kutumia sehemu kubwa ya makusanyo yake kuhudumia deni badala ya kutoa huduma kwa wananchi kwa kuwa masharti yake yanakuwa ya papo kwa papo.

Kauli hiyo ilitolewa jana jijini Dar es Salaam na Wakili Emanue Mvula (pichani), Msemaji wa Sekta ya Fedha na Uchumi wa ACT Wazalendo, alipozungumza na waandishi wa habari.

Wakili Mvula alisema taarifa ya tathmini ya uchumi wa nchi iliyotolewa mwezi Novemba mwaka jana na Benki Kuu ya Tanzania (BoT), inaonyesha kukua kwa kasi kwa Deni la Taifa huku takwimu zikionyesha ndani ya mwaka mmoja, kasi ya deni hilo imeongezeka kwa Sh. trilioni 21 kufikia Sh. trilioni 90.35 huku uchumi wa nchi ukiendelea kukua kwa asilimia 4.5.

"Kukua kwa Deni la Taifa kumeibua mjadala kutoka makundi mbalimbali. Sisi, ACT Wazalendo tulifanya uchambuzi wa ripoti ya Tathmini ya Uchumi ya mwezi Novemba 2022 iliyotolewa Desemba na BoT, pamoja na mambo mengine, tumeangazia kasi ya ukuaji wa Deni la Taifa na kasi ya uingizaji wa bidhaa kutoka nje na kushuka kwa mauzo yetu kwenda nchi zingine," alisema.

Wakili Mvula alisema kwua hadi kufikia Novemba 2020, Ripoti ya Benki Kuu inaonyesha kuwa Deni la Ndani la Serikali lilikuwa Sh. trilioni 15.9 na Novemba mwaka 2021 Deni la Ndani lilikua Sh. trilioni 18.6 na kufikia Novemba 2022 Deni la Ndani limefikia Sh. trilioni 26.6. Ongezeko hili halijawahi kutokea kwa zaidi ya miaka 20 iliyopita.

"Kiwango hiki cha Deni la Ndani ni asilimia 30 ya Deni zima la Taifa. Kwa nchi za uchumi wa chini (Low-income countries), uwiano wa Deni la Ndani kwa Deni la Taifa haupaswi kuzidi asilimia 20.

"Hivyo, tunaona kwa muda wa mwaka mmoja, kasi ya ukuaji wa Deni la Ndani ni kubwa sana kuliko wakati wowote ule katika historia ya nchi yetu," alifafanua Wakili Mvula.

Alitaja athari zingine za ongezeko la Deni la Ndani la Taifa kuwa ni serikali kulazimika kuingia sokoni kukopa zaidi ili kulipa madeni (hati fungani) yaliyoiva, huku sekta binafsi ikipata wakati mgumu wa kupata mikopo zaidi katika taasisi za kifedha kutokana na taasisi hizo kuona ni rahisi kwao kufaidika kwa urahisi kwa kuikopesha serikali.

"Mbali ya deni hili la ndani kuiminya sekta binafsi kupata mikopo kutoka taasisi za kifedha kutokana na kugombea mikopo na serikali, pia kunasababisha ongezeko la utitiri wa kodi, tozo, ushuru na makato kwenye bei za mazao ya wakulima, kucheleweshwa kwa malipo ya mafao na pensheni za wastaafu ambao ni wanufaika kunakosababishwa na fedha nyingi za mifuko hiyo kukopwa na serikali," alisema.

Wakili Mvula aliongeza kuwa ni muhimu kwa mwaka huu wa fedha katika mpango wa bajeti serikali kuja na mkakati wa namna ya kupunguza kiwango kikubwa Deni la Ndani ili kuwaondolea mzigo wananchi wa kuminywa kupitia utitiri wa kodi, tozo, ushuru na makato ya bei za mazao kwa ajili ya kulihudumia deni.

Alisema njia nyingine ni serikali kupunguza Deni la Ndani kwa kulipa kwa mkupuo madeni ya ndani na hati fungani ili kuweka uwiano sawa.

Alishauri katika kuleta uwiano mzuri wa mauzo ya nje na kupunguza kasi ya uagizaji wa bidhaa kutoka nje, serikali ichukue hatua za haraka kwa kuanza na kuongeza uuzaji wa bidhaa za kilimo kwa kuongeza thamani ya mazao kama vile kuuza korosho iliyobanguliwa.

Njia nyingine ya kupunguza Deni la Ndani kwa mujibu wa Wakili Mvula, ni serikali kuweka nguvu kubwa Mchuchuma na Liganga ili kusafirisha chuma na kupata chuma cha ndani.

"Kwa mfano, ripoti ya Benki Kuu inaonyesha tuliagiza chuma kwa Sh. trilioni 1.63 mwaka 2022 kuanzia Januari mpaka sasa," alifafanua.

Aliongeza kuwa hatua hiyo itapunguza mzigo wa serikali kugharamia madeni na hivyo kuipa unafuu serikali kugharamia sekta zingine za maendeleo ya wananchi kama vile afya, elimu, maji, umeme na kilimo.




**KOZI YA WAFANYAKAZI NDANI YA NDEGE (CABIN CREW).**

Chuo Cha Kampuni ya Ndege ya Tanzania (ATCL Training Center ) kina furaha kuwatangazia watanzania wote kuwa kwa mara nyingine kitaendesha kozi ya wafanyakazi ndani ya ndege (Cabin Crew ) kuanzia tarehe 20 February 2023. Kozi hii ni ya muda wa miezi mitatu (03), chuo kipo uwanja wa ndege wa kimataifa wa Julius Nyerere-Dar es salaam (JNIA) Terminal One kwenye jengo la utawala la ATCL karibu kabisa na kituo cha polisi uwanja wa ndege. Chuo kinakaribisha maombi ya kujiunga na kozi hii kwa wenye sifa zilizoainishwa hapo chini. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 27 Januari 2023

**Sifa za mwombaji.**

i. Awe na umri kuanzia miaka 18 hadi miaka 25
ii. Awe timamu kiakili, kimaumbile na urefu kuanzia futi 5"4 na kuendelea
iii. Elimu sio chini ya kidato cha nne na kufaulu angalao masomo manne, hasa masomo ya Kiingereza na Jiografia
iv. Aweze kuongea na kuandika kwa ufasaha lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Muombaji mwenye uelewa wa lugha zaidi ya hizi mbili kama Kiarabu, Kichina, Kihindi na Kifaransa atapewa kipaumbele.
v. Awe Mtanzania au raia wa kigeni mwenye vibali halali vinavyomruhusu kukaa na kusoma nchini.

**Angalizo:** Waombaji kutoka nchi za kigeni watatakiwa kulinganisha matokeo ya vyeti vyao kwenye Baraza la Mitihani Tanzania (NACTE) yafanane na matokeo ya Tanzania.

Barua ya maombi iambatane na vitu vifuatavyo.

i. Nakala za vyeti vya shule/chuo alikosoma
ii. Nakala ya cheti cha kuzaliwa
iii. Picha mbili ndogo (passport size) na picha moja yenye kuonyesha umbo lote ukubwa wa 6x8
iv. Curriculum Vitae –CV

**Maombi yatumwe kwa:**
**Principal**
**ATCL Training Center**
**Box no 543**
**Dar**
**Email , training@airtanzania.co.tz**
**Mob: +255735787212 , Landline: +255222842543**
**ATCL TRAINING CENTER**

***Welcomes you, to where you can Fly***

217229301

# Watoto wafundishwa kulawitiana shuleni

## - Wahusika wakuu ni wageni, butwaa mkoani hadi wizarani

**Na Mwandishi Wetu,**
MOSHI

"SHULE binafsi kuna uchafu mwingi. Baada ya mume wangu kupata uhamisho wa kituo cha kazi, nami nilikwenda masomoni, tukalazimika kuwahamishia kwenye shule ya bweni watoto wetu wawili, Selina (si jina lake halisi) anasimulia mkasa uliojaa ukakasi wa yanayojiri kwenye baadhi ya shule nchini.

Selina, mkazi wa Manispaa ya Moshi na mzazi wa watoto wawili, anaendeleza simulizi yake, akisema kuwa kutokana na uhamisho huo wa kikazi, yeye na mumewe waliwapeleka shule binafsi watoto wao wawili - wa kike (7) na wa kiume (9) na baada ya mwaka mmoja walibaini mabadiliko hasi ya kitabia, hasa kwa mtoto wao wa kiume waliyempeleka kwenye moja ya shule binafsi zilizoko Moshi Vijijini.

"Baada ya mwaka mmoja kupita, nilirejea na kuwachukua wanangu kurudi shule za kutwa. Siku moja wakati ninaendelea na majukumu yangu, nilimwona kupitia dirishani mwanangu wa kiume akimfundisha mtoto wa jirani namna ya kufanya vitendo vya ulawiti.

"Nilisononeka na kukaa na mwanangu, nikamdadisi kwa nia ya kutaka kujua wapi alikojifunza tabia hiyo.

"Mwanangu alinieleza kuwa vitendo hivyo walifundishwa na patron (msimamizi wa kiume wa wanafunzi shuleni) wa ile shule nilikompeleka kwa mwaka mmoja.

"Alinieleza kuwa walikuwa wanafundishwa vitendo hivyo nyakati za usiku na walipewa onyo wasitoe taarifa kwa wazazi wala walimu huku wakiahidiwa zawadi mbalimbali, zikiwamo kalamu na penseli pamoja na kupewa fursa ya kuzungumza na wazazi kwa simu wanapopata shida," anasimulia.

Mama huyo anasema mwanawe alimweleza kuwa msimamizi huyo wa wanafunzi huwapatia watoto mafuta maalum ya kufanyia vitendo hivyo, kukiwa na utetezi kwamba mafuta hayo yanawaepusha kupata michubuko.



Waziri wa Elimu, Sayansi na Tenolojia, Prof. Adolf Mkenda



Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dk. Fredrick Shoo.

"Mwanangu aliniambia kwamba wavulana wa darasa la sita na la saba ndiyo huja kuwafanyia vitendo hivyo wanafunzi wa madarasa ya chini.

"Patron huwaambiwa ikiwa watakubali, wataanza kupakwa mafuta ili wasiumie na wale wanaowafanyia hivyo, watawasaidia majukumu mbalimbali ikiwamo kufua, kufuta viatu kuchukuliwa chakula na kununuliwa vitu mbalimbali na wakikaidi, patron angewachukulia hatua za kinidhamu.

"Baada ya kupata taarifa hizi, imenilazimu kuchukua hatua ya kuwatafuta watu wa kiroho pamoja na kumpeleka mtoto hospitalini, sijathubutu kumweleza baba yake, ila kiukweli tunaomba vyombo vya usalama vya mkoa vichunguze kwa kina, haya matukio yapo na ni ya aibu!" Selina analalamika.

**MAJIRANI WA SHULE**

Edwad Shirima, mkazi wa Mji wa Moshi, ana angalizo lake kimaadili, akidai vitendo hivyo vinachochewa na baadhi ya wamiliki wa shule hupokea fedha kutoka kwa watu wanaofadhili vitendo vya ushoga ili kuwa sehemu ya mkakati huo.

"Kuna shule moja inasemekana mmiliki wake na walimu wachache wanapewa taarifa juu ya miradi hiyo na kunakuwa na nembo zao, ila watekelezaji ni patron.

"Kwa kweli kwa sasa hali ni mbaya, wazazi tuache kujikita katika kutafuta fedha, watoto wanaangamia," Shirima anatahadharisha.

Nehemia Munis, mfanyabiashara wa vitafunwa maeneo ya Stendi ya Moshi Mjini na mkazi wa Pasua, Manispaa ya Moshi, anasema mbali na ukatili unaofanywa na watoto kwa watoto chini ya viongozi wa shule, pia wapo vijana waendesha bajaj na pikipiki, maarufu bodaboda, ambao wamekuwa sehemu ya watu wanaowalawiti watoto wakati wanapowapeleka shuleni au kuwachukua kutoka shuleni kuwarudisha nyumbani.

"Mwaka jana watoto sita wa shule zilizopo katikati ya mji -- Muungano na Mawenzi walilawitiwa na dereva bajaj wakati wa kuchukuliwa shuleni.

"Tukiwa kijiweni siku moja, kuna mtoto akawa anatoka wadudu sehemu za siri na amekaa kwa masikitiko, tukamwita na kumhoji, akatueleza namna yeye na wenzake watano wanavyofanyiwa vitendo hivyo nyakati za kurejea nyumbani na dereva bajaj.

"Yaani huyo aliyepewa dhamana ya kuwaleta shuleni watoto, anawafanyia unyama.

Tukachukua jukumu la kumpeleka shuleni na kuanika kilichokuwa kinaendelea," Munis anasema.

Elisante Mfuru, mkazi wa Sango wilayani Moshi, anashauri kila mwanajamii hana budi kufuatilia malezi ya watoto ili kuliepusha taifa kuwa na kizazi kilichopotoka kimaadili.

"Wapo watu watadai wazazi walaumiwe, ila mimi ninasema kila mmoja anapaswa kujitafakari kwa kuwa kuporomoko kwa maadili na utandandawazi kumechangia jamii kufika hapa tulipofika leo, jamii mzima tumejisahau," alisema.

**WAZEE NA MILA**

Elisaria Nkya (79), mkazi Narumu mkoani hapa, anawasilisha uzoefu wake kwamba zamani matukio hayo ilikuwa nadra kutokea, akinyoshea kidole wazazi kupeleka shule za bweni watoto wenye umri mdogo.

"Mtoto wa miaka miwili amepelekwa shule ya bweni ili mama asichoke, mila na desturi hazifuatwi tena, vijana wa miaka kuanzia 1990 na kuendelea hawajitambui, hawafuati maadili ya Mungu wala ya kimila.

Ni kizazi kisichokuwa na maadili," anaonya.

Ni hoja inayoungwa mkono na Sebastian Kimaro (81), mkazi wa Rombo Mkuu, anayetaja kuporomoka kwa maadili, utandawazi na uvivu kwa vijana kutaka fedha za haraka kuwa chanzo cha tatizo.

"Zamani ukibainika umefanya tukio la namna hiyo (kulawiti), mwanamume unaitwa na wazee wakubwa wa ukoo, unashikishwa mbuzi kama ishara ya kuwapa na ikiwa umefanya hivyo unapaswa kufa mara tu mbuzi yule anapochinjwa.

"Hivyo, watu waliogopa kutenda, si kwa watoto tu, bali hata kwa wake zao japo wachache walikuwapo wenye tabia za kijinga kama hizi," anasema Zakaria Shirima (78), mkazi wa Kibosho Umbwe.

**HATUA SERIKALINI**

Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro, Wily Machumu anakiri wamepata taarifa za matukio ya ukatili wa aina hiyo dhidi ya watoto kwenye baadhi ya shule binafsi na tayari wameanza uchunguzi wa kina ili kubaini ukweli wa jambo hilo kuchukua hatua stahiki za kisheria.

"Tumepata taarifa za kuwapo matukio ya kikatili hasa katika baadhi ya shule binafsi zilizopo mkoani hapa, tunafanya uchunguzi wa kina ili kubaini shule hizo na kuzichukulia hatua za kisheria.

"Pia tunaendelea kutoa elimu ya kina juu ya kutambua wajibu wao na kuwa walinzi wa watoto chini ya Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009. Serikali mkoani hapa hatutavumilia kuona mtu anafanya ukatili, viongozi wa dini watusaidie, jamii tubadilike," anahimiza.

**KATIBU TAWALA.**

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu analaani ukatili huo dhidi ya watoto na kuwaomba wabunge wa mkoa huo kwenda bungeni kuwasilisha hoja ya kubadilisha sheria ya adhabu dhidi ya wanaofanya vitendo hivyo. Anasema kuna tatizo la mmomonyoko mkubwa wa maadili, akifafanua kuwa watu wamegeuka kuwa wanyama, wakitenda mambo kama hawana akili.

"Tuna kesi kadhaa katika mkoa wetu, jitu zima lina akili, linakwenda kumchukua mtoto wa miaka 10, anakusaidia nini? Wanawake wapo wengi na wengine hawajaolewa, kwanini usiende kuoa na kukaa na mke wako?" Babu anahoji. Anaongeza: "Mkoa wa Kilimanjaro umekithiri vitendo vya ukatili wa kijinsia, hali ni mbaya kwa sasa. Na zipo pia shule ambazo hutumia alama maalum za ushoga, nimeshawaita wamiliki wa shule hizo kujieleza."

Waziri wa Elimu, Sayansi na Tenolojia, Prof. Adolf Mkenda anasema wizara yake kwa kushirikiana na viongozi wa dini na wazazi, ina jukumu kubwa la kuzuia vitendo vya ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto vinavyoendelea kwa kasi nchini.

"Tumekuwa tukisikia visa vingi vya unyanyasaji wa kijinsia, sijui ni kwa sababu sasa ni rahisi sana kupata taarifa au dunia imeharibika zaidi. "Vyovyote vile, tuna jukumu la kuhakikisha tunazuia vitendo hivi. Tunajua watoto wamekuwa wakitumia muda mrefu shuleni na (shule) nyingine ni za kulala, hivyo bado wizara inaendelea kutafakari," anasema Prof. Mkenda wa kusisitiza kuwa kila mmoja ana jukumu la kuhakikisha anakuza maadili ya watoto.



Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu.

Msemaji wa Jeshi la Polisi, David Misime katika mazungumzo na Nipashe kuhusu suala hilo, anasema wamejipanga kuwapa mafunzo askari na wakaguzi wao ili kuendana na wakati, akisisitiza utendaji wa uhalifu umebadilika kutokana na kukua kwa sayansi na teknolojia.

Anabainisha kuwa Desemba 31 mwaka jana, Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini alitoa nafasi kwa askari na wakaguzi 29 kwenda India kwa ajili ya mafunzo ya unyanyasaji wa watoto katika mitandao na kushughulika na makosa ya kimtandao.

"Tutaendelea zaidi kuhakikisha askari na maofisa wetu wanapata elimu na weledi zaidi wa kuzuia uhalifu na kupeleleza kesi pale zinapotokea," Misime anasema.

**VIONGOZI WA DINI**

Katibu Mkuu wa Baraza la Waisilamu, Nuhu Mruma anasema wanaendelea kupingana na ukatili dhidi ya watoto na wanawake, wakitoa elimu kuhusu kufuatilia na kutoa taarifa za matukio yote ya ukatili.

Askofu wa Jimbo Katoliki la Moshi, Ludovick Minde anautaja utandawazi, watu kukosa maadili na wazazi kujikita katika shughuli za kimaendeleo zaidi kuliko malezi ya familia, kuwa ni miongoni mwa vichochea vya matukio ya ukatili.

"Familia hazina muda wa kusali kwa pamoja. Sisi kama kanisa na Jimbo Katoliki Moshi tutaendelea kupinga ukatili wowote ule utakaofanywa na mtu yeyote yule," anasema Askofu Minde.

Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dk. Fredrick Shoo anaiambia Nipashe kuwa ukatili umekithiri nchini, akiwataka viongozi wote kusimama kutokomeza tatizo hilo. "Wanadamu wote tuchukie ukatili, mwalimu ona uchungu kuharibu mtoto wa mwenzako, tuache kuiga mila za kigeni, vijana acheni kupenda fedha za haraka na kufanya matukio ya ushirikina, wazazi na walezi tuwatunze watoto," anahimiza Askofu Dk. Shoo.




Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), Nicodemus Mkama akigonga kengele kurasimisha kuorodheshwa kwa hatifungani ya Fursa Sukuk katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE). Kushoto ni Shekhe Mohamed Issa kutoka Kituo cha Masuala ya Fedha ya Kiislamu (CIFCA) akifuatiwa na Mkuu wa Idara ya KCB, Sahl Banking, Amour Muro. Kulia kabisa ni Mkuu wa Masoko, Uhusiano na Mawasiliano wa benki hiyo, Christine Manyenye akifuatiwa na Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa DSE, Mary Mniwasa. **PICHA: MPIGA PICHA WETU.**

# Nauli mpya za DART kuanza rasmi leo, wanafunzi kicheko

**Na Joseph Mwendapole**

WAKALA wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salam (DART) umetangaza ongezeko la nauli za usafiri huo kuanzia leo Jumatatu.

Mabadiliko hayo ya nauli hayatawagusa wanafunzi ambao wataendelea kulipa nauli ya Sh. 200 kwa ruti watakazokwenda.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na kutiwa saini na Meneja Uhusiano, William Gatambi, wameanza kutumia nauli hizo mpya baada ya kuidhinishwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA).

Taarifa hiyo ilibainisha kuwa mabadiliko ya nauli hizo ni kwa mujibu wa sheria ya iliyoipata LATRA mamlaka ya kupanga nauli kwa vyombo vya moto vinavyotoa huduma ya usafiri wa ardhini.

Ilifafanua zaidi kuwa mabadiliko ya nauli hizo ni kwa watu wazima tu wanaotumia njia kuu (route) na njia za mchepuko (feeder routes)

Taarifa hiyo ya DART ilibainisha kuwa nauli mpya ya Sh. 750 itatumika kwa ruti za kwenda na kurudi Kimara-Gerezani, Kimara-Moroco, Ubungo-Kivukoni, Ubungo-Gerezani, Moroco-Kivukoni, Moroco-Gerezani na Gerezani-Muhimbili.

Taarifa hiyo ilibainisha kuwa safari ya Kimara-Mbezi nauli itakuwa Sh. 500 na Kimara-Kibaha na Kimara kwenda Mlonganzila nauli mpya itakuwa Sh. 700.

Mabasi ya DART yanahudumia watu 180,000 kwa siku huku bado kukiwa na malalamiko ya wananchi kukaa muda mrefu vituoni kusubiri usafiri huo wakati wa kwenda na kurudi kazini.

Akizungumzia suala hilo Oktoba 4 mwaka jana, Mkurugenzi Mtendaji wa DART, Dk. Edwin Mhede alisema wanatarajia kuongeza mengine 177 ndani ya miezi sita.

Alisema wakati wowote DART itatia saini mkataba na mzabuni na baada ya kutia saini, mabasi hayo yatawasili nchini ndani ya kipindi cha miezi sita na kuanza kutoa huduma kwenye sehemu watakazokubaliana.

"Usanifu wa mradi wa mwendokasi wakati unaanza makadirio yalikuwa mabasi 305 na sasa tunayo mabasi 210 lakini yaliyopo hayatoshelezi mahitaji, ndiyo sababu tunatarajia kuongeza mengine 177 hivi karibuni," alisema

Dk. Mhede alisema kutokana na mahitaji ya watu, DART iliamua kupeleka huduma hiyo kutoka Muhimbili kwenda Mlonganzila ili watu wanaougua au kuuguza waende kwenye hospitali hizo kwa urahisi.

Alisema mahitaji ya usafiri huo yaliwalazimisha kupeleka usafiri huo Kibaha mkoani Pwani na kwa sasa wanatoa huduma kwa makundi maalum kama ya wazee na wenye changamoto za maumbile.

Alisema kwa sasa mabasi yao yanatoa huduma kwa watu 180,000 kwa siku lakini baada ya kuwasili kwa mabasi mengine, idadi hiyo itaongezeka mara dufu na yatapunguza muda wa msafiri kukaa kusubiri basi.

Mwaka jana DART ilisema wateja wa mabasi hayo wataanza kutumia kadi janja kununua tiketi kuanzia Februari mwaka huu kama hatua ya maboresho.

Meneja wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) wa Wakala, Ng'wananashigi Gagaga alisema ununuzi wa tiketi kwa kutumia kadi janja utawarahishia watumiaji wa usafiri huo kutolazimika kukaa foleni muda mrefu kwa ajili ya kukata tiketi, hivyo kuwaondolea adha ya kupoteza muda kwenye vituo hivyo.

Alisema mfumo huo wa kukusanya nauli kupitia kadi janja umesanifiwa na kutengenezwa na wataalamu wa ndani kutoka DART, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Wizara ya Fedha na Mipango na Serikali Mtandao.

# Mwalimu wa madrasa mbaroni tuhuma kunajisi wanafunzi

**Na Samson Chacha,** TARIME

MWALIMU wa madrasa kwenye Msikiti wa Kebeyo, Kijiji cha Getenga, Tarafa ya Inchugu wilayani Tarime mkoani Mara, Shaban Harun (37) anashikiliwa na Jeshi la Polisi Kituo cha Sirari kwa tuhuma za kuwanajisi wanafunzi wake wawili wenye umri wa miaka minane kila mmoja.

Inadaiwa kuwa mwalimu huyo alifanya ukatili huo dhidi ya watoto hao (majina tunayahifadhi) baada ya kuwapeleka kwenye chumba anachoishi na kuwafanyia vitendo hivyo.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Getenga, Julius Makuri alidai: "Wakazi wa Kitongoji cha Kebeyo, Kijiji cha Getenga tumesikitishwa na kitendo cha mwalimu huyo kuwatendea vitendo vya kinyama watoto wadogo ambao ni wanafunzi wake.

"Tunaomba sheria ichukue mkondo wake ili iwe fundisho kwa watu wengine wenye nia mbaya dhidi ya watoto ambao ni taifa la kesho."

Wazazi wa watoto hao Magreth Sabai na Joyce Gesere, walikutwa na Nipashe wakiwa na watoto wao, nje ya Kituo cha Polisi Sirari.

"Watoto wetu ni wanafunzi wa madrasa katika Msikiti wa Kebeyo uliopo jirani kwetu tunakoishi na wote wana umri wa miaka minane," Magreth alisema na kufafanua:

"Mnamo Alhamisi jioni wiki hii (wiki iliyopita), nikiwa nyumbani nilisikia sauti ya mtoto wangu na mwenzake wakilia, wakiomba msaada sauti ilitoka chumba cha mwalimu wa madrasa.

"Nilitoka ndani kwangu na kwenda walikokuwa watoto wakilia na kuomba msaada. Nilifika na kugonga mlango kisha kuingia moja kwa moja hadi ndani ya chumba cha Maalim Shaban na kuwakuta watoto wawili, mmoja wa kwangu na mwingine wa Joyce Gesere wakilia kutokana na maumivu waliyopata kwa kubakwa na mwalimu Shaban.

"Na hapo nilipiga yowe kuomba msaada kutoka kwa majirani na mara moja watu walijitokeza na kumkamata Mwalimu Shaban na watoto hao tukawakimbiza kuwapeleka Kituo cha Polisi na kupatiwa barau ya matibabu (PF3) na kwenda Hospitali ya Tarafa ya Sirari na kupelekwa Hospitali ya Wilaya ya Tarime kupata matibabu na kufanyiwa uchunguzi zaidi, tulifungua jalada la ubakaji namba SIR/RB124/2023."

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tarime/Rorya, Geofrey Sarakikya alithibitisha kukamatwa kwa mtuhumiwa huyo kwa madai ya kuwanajisi watoto hao wawili wa Kijiji cha Getenga.

"Mtuhumiwa Shaban anashikiliwa na jeshi letu na anahojiwa kuhusian na tuhuma zinazomkabili za ubakaji watoto wawili. Uchunguzi ukikamilika atafikishwa kwenye vyombo vya sheria kwa hatua zaidi.

"Jeshi la Polisi linatoa wito kwa jamii kutoa ushirikiano kwa kutoa taarifa za uhalifu kwenye maeneo yao ili hatua zichukuliwe mapema kabla ya tukio kufanyika. Tunalaani vitendo hivyo vya ukatili dhidi ya watoto," alisema.

**Summons to appear (O.VR.20 (1) of (CPC)**
**(Substituted Service)**

**IN THE COURT OF TANZANIA DAR ES SALAAM**
**(LAND DIVISION)**
**MISC. LAND APPLICATION NO. 769 OF 2022**

**RUTH JACKSON MPUNDA............APPLICATION**
**VERSUS**
**THE COMMISSIONER FOR LANDS & OTHERS......**
**RESPONDENT**

**TO; YUSUPH MZEE NGORORO**
**P.O. Box 534, DAR ES SALAAM.**

**WHEREAS:** The above named APPLICANT has institute the **APPLICATION** against you, you are hereby summoned to appear in this court in person or by advocate or authorized Agent on 25TH day of **JANUARY, 2023 at 09:00 AM** Before **HON. T. MWENEGOHA, JUDGE,** to answer the said PLAINT and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your **REPLAY.**

**TAKE NOTICE** that, in default of your appearance on that day the said APPEAL will be heard and determined in your absence.

Given under my hand and the seal of this court, this **4TH day of JANUARY, 2023.**

DEPUTY REGISTRAR

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) MBINGA**
**SHAURI LA MADAI NAMBARI 95/2022**
**FULKO C. KAPINGA....MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**MATHIAS NCHIMBI...........MJIBU MAOMBI**
**WITO/KUITWA SHAURINI**
**MDAIWA MATHIAS NCHIMBI POPOTE ULIPO.**

**BW FULCO C. KAPINGA** amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo (Boma). Shauri husika limepangwa kusikilizwa tarehe 02/02/2023. Hivyo basi unatakiwa kuleta utetezi wako ndani ya siku 21 kuanzia tarehe ya tangazo hili kutolewa. Vielelezo vyote vya kesi vinapatikana katika masijala ya wazi Baraza la Ardhi na Nyumba (W) Mbinga.

Endapo hutatekeleza haya shauri litasikilizwa upande mmoja na hukumu kutolewa.

**AMRI** hii imetolewa kwa mkono wangu na Lakiri/ Muhuri wa Baraza hili leo hii tarehe 09 mwezi 01 mwaka 2023.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) MBINGA

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Klabu zimegharamika dirisha dogo, waamuzi tendeni haki

**RASMI** usajili wa dirisha dogo Ligi Kuu Bara, Championship na First League, lililokuwa wazi tangu Desemba 16, mwaka jana, limefungwa jana saa sita usiku na tayari baadhi ya wachezaji waliosajiliwa walishaanza kuzitumikia timu zao mpya kuanzia raundi ya 19 ya Ligi Kuu.

Hata hivyo, kwa upande wa Ligi Kuu Bara, ushindani umezidi kuwa mkubwa na licha ya Yanga kuwa kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo ikiwa na alama sita zaidi ya Simba inayoshika nafasi ya pili na 10 zaidi ya Azam iliyopo nafasi ya tatu ikiwa na pointi 40, bado hilo haliwezi kuihakikishia kutwaa ubingwa.

Lakini pia zipo timu zinazowania kumaliza nafasi nne za juu na zile zinazopigana vikumbo kuepuka kushuka daraja wakati huu Ruvu Shooting ikiburuza mkia kabla ya mechi yao ya jana dhidi ya Coastal Union inayoshika nafasi ya tatu kutoka mkiani ikiizidi Polisi Tanzania kwa alama tatu, ambayo ipo nafasi ya pili kutoka chini.

Hivyo, dirisha la usajili lililofungwa jana usiku, ni wazi litakuwa limezisaidia klabu nyingi kujiimarisha katika nafasi mbalimbali wakati huu ligi hiyo ikielekea hatua za lala salama na kila timu ikihitaji kupambana kupata matokeo ili kufikia malengo yake iliyojiwekea mwanzoni mwa msimu.

Pamoja na yote hayo, tunatambua waamuzi wamekuwa kero kubwa katika kutenda haki uwanjani, na kuzifanya baadhi ya timu kupoteza ushindi pasipokustahili huku zingine zikinufaika na ufinyangaji huo wa sheria 17 za soka.

Hivyo, tunapenda kuwakumbusha waamuzi kuwa timu zinatumia gharama kubwa sana katika kusajili wachezaji, kuwalipa mishahara pamoja na posho mbalimbali, hivyo mtu mmoja tu kusimama kwa matakwa yake mwenyewe na kuamua kutoa ushindi kinyume cha sheria 17 za soka, hilo halikubaliki.

Ni wakati sasa kwa kila mwamuzi anayepewa dhamana ya kuchezesha mechi, kutenda haki na ionekane ikitendeka kweli, kwani alama tatu ama moja tu katika mchezo mmoja inaweza kuwa chanzo cha timu kumaliza nafasi isiyostahili na matokeo yake kusababisha kupatikana bingwa batili, mshindi wa pili, tatu wa nne na hata zinasoshuka daraja kuathirika.

Tunataka kuona timu inayoshinda ikishinda kihalali ili mwisho wa msimu tupate wawakilishi bora kwenye michuano ya kimataifa, lakini pia timu zinazobaki Ligi Kuu ziwe zilizostahili nafasi hiyo jambo ambalo litaifanya ligi yetu kuendelea kuwa moja kati ya ligi bora barani Afrika na kuvutia wachezaji wengi zaidi wa kigeni kuja kucheza soka nchini.

Wote tunashuhudia kwa sasa wachezaji wengi wa kigeni kutoka Afrika Magharibi na wengine wakihama kutoka walipokuwa wanacheza timu za Afrika Kaskazini na kuja kucheza soka nchini, hiyo yote inatokana na uwekezaji mkubwa unaofanywa na wadau wa soka, lakini hayo yote yanaweza kutoweka endapo maamuzi ya waamuzi yataendelea kuwa kero uwanjani.

Tumelazimika kulisema hilo mapema kutokana na kutambua kwamba karibu kila msimu nyakati kama hizi, Ligi Kuu Bara ikielekea ukingoni, ndipo madudu makubwa ya uvunjifu wa sheria 17 za soka hufanywa na waamuzi kwa manufaa na dhamira zao wenyewe. Hivyo, Bodi ya Ligi Tanzania (TPLB), ikishirikiana na Kamati ya Waamuzi chini ya Chama cha Waamuzi nchini (FRAT), hawana budi kuongeza makali yao kwa kila atakayebainika kuchezesha kinyume cha sheria 17 za soka duniani, kwani hilo litasaidia ligi yetu kuendelea kuwa kivutio zaidi Afrika.

Katika hilo, pia tunalikumbusha Shirikisho la Soka nchini (TFF), pamoja na TPLB, kama kuna malimbikizo ya malipo kwa waamuzi yamalizwe na kuanza kuwalipa kwa wakati ili kuwafanya waifurahie kazi yao jambo litakaloweza pia kupunguza vishawishi vinavyoweza kujitokeza katika ufinyangaji wa sheria 17 za soka.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Tatizo la mastraika Tanzania linahitaji mjadala, lakini...

**WALA** tusipindishe kona kona, tuseme ukweli tu kuwa kuna tatizo kubwa kwa mastraika wa Kitanzania ambalo wengi hawataki kukiri na hakuna juhudi zozote za kulifanyia kazi.

Baadaye tukizinduka kuna mtu atakuja na kusema tuzuie mastraika kutoka nje ya nchi wasiingie badala yake tutumie wa hapa hapa ili viwango vyao vipande, au tupunguze kila timu iwe na straika mmoja tu kutoka nje kwa ajili ya kulinda vipaji.

Ndivyo baadhi ya Watanzania tulivyo, kwa sababu hata wachezaji hawa tu kutoka nje wapo watu ambao hawawataki, na wengine wanaona wangepunguzwa tu. Hawa ni wale wanadhani kipaji cha mtu kinaonekana baada ya mwenye kipaji kikubwa zaidi yake kubanwa au kuondolewa tu.

Hawadhani kuwa kipaji huwa kinaonekana kwa kushindana na mwenye kipaji kikubwa zaidi yake. Nimekuwa nikiangalia ligi kwa muda mrefu, lakini kadri miaka inavyozidi kusonga mbele naona Tanzania inakwenda kuishiwa mastraika.

Nikisema mastrika nina maana halisi ya wale waliokamilika, wenye uwezo wa kucheza mbele pale akisumbua mabeki na kupachika mabao.

John Bocco ndiye straika halisi wa Kitanzania ambaye ndiyo hivyo wakati wake unaondoka. Na cha ajabu pamoja na umri kumtupa mkono na kucheza mechi chache sana, tayari amewapita washambuliaji wengi wa Kitanzania ambao ni vijana.

Ana mabao tisa, akiwa anatoka kwenye majeraha, lakini pia kwa sasa si mchezaji wa kutegemewa sana kwenye timu yake. Bocco ndiye straika pekee wa Kitanzania ambaye msimu wa 2008/09 alipoanza kucheza Ligi Kuu amekuwa akifunga mabao kuanzia 10 kwenda mbele kwa misimu yote mfululizo akiwa Azam hadi Simba.

Hakuna straika yeyote wa Kitanzania ambaye ameweza kufanya hivyo hata kwa misimu miwili tu. Tulikuwa na kina Abdulrahman Mussa, Salum Aiyee, Adam Adam, Meshack Abraham, Waziri Junior, Yusuph Mhilu, Marcel Boniventure Kaheza, Mohamed Rashid, Habib Kyombo, Elius Ambukile, Mbaraka Yusuph, Kelvin Sabato, Shaaban Chilunda na wengine wengi sana.

Hawa wote kwa sasa mashabiki wengi walitarajia kuwa wangekuwa mbadala wa Bocco kwa jinsi walivyokuwa wakifanya vizuri huko nyuma kila mmoja kwa nyakati tofauti, lakini walikuwa wakiwika na kupachika mabao mengi kwa msimu mmoja mmoja tu, viwango vyao vinashuka.

Pamoja na kwamba wameendelea kuwa kwenye Ligi Kuu, lakini huwa hawarudii tena kufanya kama walivyofanya huko nyuma na kumuacha Bocco pamoja na ukongwe wake akiendelea kuwa na kiwango kile kile na kuwa na wastani ule ule wa mabao kila msimu na hata kuzidi.

Kwa ninavyoona Bocco anaweza kucheza tena hata kwa misimu mingine miwili na kuwazidi mabao mastraika vijana tulionao. Inashangaza kuona mastraika kutoka nje ndiyo wanaokuja kufanya kazi hiyo na wanaifanya vizuri sana. Yanga kuna Fiston Mayele na Simba kuna Mosses Phiri. Singida Big Stars kuna Meddie Kagere na wameshamleta Kazadi Kasengu ambaye ameonyesha uwezo mkubwa kwenye Kombe la Mapinduzi. Hata timu za majeshi ambazo zamani huwezi kuona wanaleta wageni, lakini sasa wameamua. Polisi Tanzania imemchukua straika Mkongomani Enock Mayala na juzi tu akicheza mechi ya kwanza amefunga mabao mawili dhidi ya Namungo, ikishinda mabao 2-0.

Kwenye Ligi ya Championship nako kuna Mkongomani anatupia kweli, anaitwa Ngoi wa Ngoi Fabrice. Hii inaleta ushawishi kwa klabu zingine kusajili mastraika kutoka nje kwa sababu wa hapa ndani wameonekana kushindwa.

Haikubaliki na haipendezi straika anamaliza ligi ana mabao matano tu. Kuna sehemu tunakwama. Labda kwa sasa vipaji hivyo havipo, au mafunzo madogo wanakotoka, maumbo ya wachezaji wa sasa wa Kitanzania, au wachezaji wa sasa wanapenda sana kuuchezea mpira na kupiga sana chenga kiasi kwamba hawazalishwi wengi kwenye nafasi hiyo.

Nashangaa hata kwenye Ligi Kuu, ni mastraika hawa hawa tu ndiyo wanapishana, msimu huu huyu akienda huku, huyu kule na wanafanye vile vile. Nilitegemea waanze kupatikana mastraika wapya kwenye klabu zetu ili nao tuwaangalie, lakini kinachoonekana nchi inazalisha zaidi mabeki wa pembeni na viungo tu.

Kwa sasa unahitajika mjadala, uchunguzi na ufumbuzi kwa ajili ya kuzalisha tena mastraika si kuwaondoa au kuwazuia wa kigeni wasiingie. Nadhani hata hii kuingia wengi nchini na kuwafundisha jinsi gani ya kupachika mabao, inaweza pia ikawa somo kwa wanaosaka na kulea vipaji vya wachezaji wetu.

**HABARI KITAIFA**

# Mkenda: Mitaala itatoa kipaumbele wanafunzi wenye mahitaji maalum

**Na Mwandishi Wetu,** MASASI

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda amesema kupitia mchakato unaoendelea wa mapitio ya sera ya maboresho ya mitaala, wanafunzi wenye mahitaji maalum watapewa kipaumbele zaidi.

Mbali na kuahidi serikali kuwapa kipaumbele wanafunzi wenye mahitaji maalum, Waziri Mkenda pia ametoa wito kwa wazazi na wadau wa maendeleo kuona umuhimu wa kuchangia juhudi za serikali katika kuwapatia huduma stahiki wanafunzi wenye mahitaji maalum ili kuwawezesha kushiriki kikamilifu katika mchakato wa ujifunzaji.

Prof. Mkenda alitoa kauli hiyo jana wilayani Masasi mkoani Mtwara wakati wa uzinduzi wa majengo mapya ya Shule Jumuishi ya Mfano ya Msingi Lukuledi na kutaja baadhi ya huduma zitakazopewa kipaumbele ni pamoja na bima za afya, vifaa saidizi, kuwajengea mabweni, kuwalipia ada na posho za kujikimu masomoni.

Waziri Mkenda pia aliwataka wazazi wenye watoto wenye mahitaji maalum, kutowaficha watoto ndani badala yake wawapeleke shuleni kwa kuwa zipo shule maalum kwa ajili ya watoto hao.

"Katika mchakato wa mapitio ya sera na maboresho ya mitaala, suala la elimu jumuishi limetiliwa mkazo na tutaendelea kutilia mkazo hadi pale litakapokamika," aliongeza Waziri Mkenda.

Mkurugenzi wa Elimu Maalum kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Magreth Matonya alisema shule hiyo ni jumuishi na inachukua wanafunzi wenye mahitaji maalum na wasio na mahitaji maalum.

Aliongeza kuwa ujenzi wa shule hiyo umegharimu zaidi ya Sh. bilioni 1.4 na ina uwezo wa kuchukua wanafunzi 320 kwa mara moja.

Alitaja baadhi ya majengo yaliyopo kwenye shule hiyo kuwa ni mabweni manne, madarasa 12, ofisi sita, nyumba za watumishi nane, karakana tatu, bwalo na jiko.

Vingine ni jengo la utawala, nyumba ya mkuu wa shule, matundu ya vyoo tisa na chumba cha upimaji usikivu.

Awali Mratibu wa Mradi wa ESPJ, Margaret Mussai aliwataka walimu, wanafunzi na wanajumuiya wa shule hiyo kuhakikisha wanatunza miundombinu ya shule hiyo ili itumike mpaka vizazi vijavyo ikiwa kwenye hali nzuri.

"Serikali imetumia fedha nyingi sana kujenga majengo haya hivyo niwaase walimu, wanafunzi na wanajumuiya wa shule hii kuitunza na kuienzi hii miundombinu ili itumike na kizazi cha sasa na cha baadaye," alifafanua Mussai.

Katika hafla hiyo, Waziri Mkenda pia alikabidhi rasmi shule hiyo kwa Ofisi ya Rais - TAMISEMI ambapo Katibu Tawala wa Mkoa wa Mtwara, Abdalla Malela alipokea Hati ya Makabidhiano ya shule hiyo.




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama (katikati) akikata utepe wakati wa uzinduzi wa Mfuko wa Faida (Faida Fund), uliofanyika kwenye ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Julius Nyerere (JNICC), jijini Dar es Salaam, Januari 14, 2023. Pamoja naye ni Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro (watano kushoto), Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deo Ndejembi (wanne kushoto), Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Dk. Natu El-Maamry Mwamba (watano kulia) pamoja na viongozi wengine. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Waziri aagiza wananchi kuunganishwa Faida Fund

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama amezitaka taasisi zinazohusika na maendeleo ya vijana, wanawake na makundi maalum, kuanza kuhamasisha makundi hayo kuwekeza kwenye mfuko wa Faida Fund.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mfuko huo uliopo chini ya Watumishi Housing mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, Waziri Mhagama alisema serikali isingependa kuona Watanzania wanaachwa nyuma katika shughuli za uwekezaji na ukuzaji wa mitaji.

Waziri huyo alitoa pongezi kwa shirika la uwekezaji katika makazi la Watumishi Housing kwa kuja na ubunifu huo ambao si tu unatoa fursa ya wananchi kuwekeza kwa faida nzuri, bali pia unasaidia shirika hilo kupata mtaji wa utekelezaji wa miradi yake ya maendeleo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Watumishi Housing, Dk. Fred Msemwa alisema uanzishwaji wa mfuko huo unatokana na maoni ya wawekezaji ambao wamekuwa wakipendelea kuwekeza mitaji yao kwa muda mfupi.

Dk. Msemwa alisema pamoja na mafanikio makubwa ya mfuko wa awali wa uwekezaji katika sekta ya makazi (WHC-REIT) uliozinduliwa mwaka 2014 na kukusanya zaidi ya Sh. bilioni 59, baadhi ya wawekezaji hususan wawekezaji binafsi wamekuwa wakiomba kuanzishwa kwa mfuko utakaotoa fursa kwa wawekezaji wengi zaidi.

"Kwa kuwa hili ni shirika la kizalendo, tuliazimia kuyafanyia kazi maoni ya wawekezaji wetu. Leo hii tunajivunia kuzindua mfuko huu wa uwekezaji wa pamoja wa Faida Fund.

"Mfuko huu haubagui kiwango cha chini cha uwekezaji hivyo unatoa fursa kwa mtanzania yeyote kujiunga," alisema Dk. Msemwa.

Mkurugenzi huyo wa Watumishi Housing aliishukuru Benki ya CRDB ambayo ni msimamizi wa mfuko huo pamoja na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali, kampuni ya sheria ya Abenry Advocates na Solomon Brokers kwa namna ambavyo wameshirikiana katika kuanzishwa kwa mfuko huo.

Akizungumza kwa niaba ya washirika wa mfuko huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela aliishukuru Watumishi Housing kwa kuipa benki hiyo fursa ya kuwa msimamizi wa mfuko huo na kubainisha kuwa benki hiyo imejipanga kuhakikisha Watanzania wote wanafikiwa na kunufaika na fursa hiyo.

Akielezea faida ya mfuko huo, Nsekela alisema ni wa kipekee kwa kuwa umezingatia sera mahususi ya huduma jumuishi za kifedha zinazomjali Mtanzania wa rika zote ikiwa ni pamoja na kununua vipande kwa Sh. 10,000, jambo ambalo linaenda sambamba na sera ya benki hiyo ya kuongeza ujumuishi wa kifedha.

Alifafanua kuwa mfuko wa Faida Fund unakuwa mfuko wa saba katika mifuko ya uwekezaji wa pamoja. Alisema benki hiyo imejipanga kusimamia mfuko huo kikamilifu na kuhakikisha maslahi ya wawekezaji yanalindwa.

Nsekela alimweleza Waziri Mhagama kuwa benki hiyo inajivunia kuwa kinara katika huduma bora za uwekezaji katika masoko ya mitaji. Alibainisha kuwa Benki ya CRDB inachangia zaidi ya asilimia 70 ya wateja wote wanaoshiriki katika masoko ya mitaji na dhamana.

Mwaka jana Benki ya CRDB ilitunikiwa tuzo na Soko la Hisa la Dar es Salaam kwa kuitambua benki hiyo kama kinara wa huduma bora kwenye masoko ya mitaji.

Benki hiyo inatoa huduma ya kuuza na kununua bidhaa zote za masoko ya mitaji kupitia mtandao wa matawi yake kote nchini.

**KABWELA** **Na Fadhili Mohammed**





Mkuu wa Wilaya ya Mkalama, Sophia Kizigo (kushoto), akimkabidhi kishikwambi Ofisa Elimu Msingi Wilaya ya Mkalama, Jamhuri Kidumu ambacho ni kati ya vishikwambi 706 walivyokabidhiwa Maofisa Elimu kata, Walimu wa Shule za Sekondari na Msingi wilayani humo ili kurahisisha majukumu yao.
**PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Mradi wa EBARR ulivyowatoa kimaisha wananchi Mvomero

**Na Lusekelo Philemon**

WILAYA ya Mvomero ni moja kati ya wilaya zinazotekeleza Mradi wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi kwa Kutumia Mifumo Ikolojia Vijijini (EBARR) ulio chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira).

Katika utekelezaji wa mradi huo, Wizara ya Kilimo inasimamia eneo la kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi na halmashauri ya wilaya ni mtekelezaji wa shughuli za mradi. Mradi huu kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero ulianza kutekelezwa mwaka wa fedha 2019/20.

Mradi unatekelezwa kwenye vijiji vitano vya Melela, Magali, Lukenge, Mingo na Lubungo ambapo utekelezaji huu ulizingatia mgawanyiko wa kiikolojia katika wilaya huku ukielekezwa zaidi kwenye maeneo yenye asili ya uhaba wa mvua na yakiwa yameathiriwa zaidi na mabadiliko ya tabianchi kutokana na shughuli za kibinadamu na majanga ya asili. Uchaguzi wa vijii hivyo ulitokana na utafiti uliofanyika ambapo vijiji hivyo vilikidhi haja ya mradi.

Shughuli za mradi katika Wilaya ya Mvomero zilikubalika baada ya kuibuliwa na wananchi wanufaika katika vijiji mwaka 2019 ambazo ni pamoja na uchimbaji wa visima (4) kwa ajili ya shughuli za kilimo, mifugo na matumizi ya majumbani, uchimbaji wa lambo (1) kwa ajili ya kuvuna maji kwa shughuli za kilimo, mifugo na majumbani, ujenzi wa mfereji mkuu wa umwagiliaji katika skimu ya Lukenge na uenezaji wa teknolojia ya matumizi ya majiko banifu na matumizi ya nishati mbadala.

Shughuli nyingine zilizoibuliwa ni uanzishwaji wa mashamba darasa ya kitalu nyumba (4), uboreshaji wa mbuzi wa maziwa, ujenzi wa josho (1) la kuogeshea mifugo, uanzishwaji wa vikundi vya uzalishaji katika vijiji, uopoaji wa maeneo yaliyoathiriwa na mabadiliko ya tabianchi na ujenzi wa kituo cha kukusanyia maziwa.

Mabadiliko ya tabianchi yamesababisha uhaba wa unyevu katika mabonde yaliyokuwa yakitumiwa na wananchi kwa shughuli za kilimo na ufugaji kipindi cha kiangazi.

Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Mratibu wa Mradi wa EBARR Wilaya ya Mvomero, Baraka Mteri anasema mradi umetumia mbinu ya kiikolojia ya matumizi ya maji yaliyomo ardhini (uchimbaji wa kisima) ambapo yatawezesha shughuli za kilimo na/au mifugo kuendelea hata kipindi cha kiangazi na hivyo kuwa suluhisho la upatikanaji wa unyevu (maji) kwa shughuli za uzalishaji.

Kazi ya uchimbaji wa visima katika Kijiji cha Mingo na Magali imekamilika na kwa sasa wananchi wanachota maji kwa matumizi ya majumbani na wengine wakiendesha shughuli zakilimo kwa kutumia maji hayo.

Mteri anasema lengo la kuchimba visima hivyo ni kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi yaliyopelekea maeneo ya mabondeni walikokuwa wanalima wananchi hao kukauka na sasa kuwa eneo kame, hivyo wao kushindwa kuzalisha mazao ya mboga kama walivyokuwa wanazalisha zamani.

Anasema mradi wa visima virefu unanufaisha wananchi takribani 1,350 katika vijiji vya Magali na Mingo. Jumla ya hekta 78 zitamwagiliwa na kuzalisha mboga kwa kutumia maji ya kisima.

Moja kati ya teknolojia inayoaminika kufanya vizuri katika afua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ni kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi, ambapo matumizi sahihi na bora ya maji ni mojawapo ya afua za kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi.

Mteri anasema kwa kutambua hilo, mradi umewezesha ujenzi wa mfereji mkuu wa umwagiliaji katika Skimu ya Lukenge ambayo tangu mwaka 2012 ilipojengewa banio na miradi ya ASDP1 hakukufanyika ujenzi wa mfereji.

"Kwa sasa ujenzi wa mfereji umefikia mita 1,200 kati ya 2,750 huku kigawa maji namba moja kikiwa kimekamilika na kina uwezo wa kumwagilia hekta 125. Mradi wa umwagiliaji ukikamilika utanufaisha wananchi 3,100," anasema.

Katika kueneza teknolojia ya matumizi ya majiko banifu na matumizi ya nishati mbadala, Mteri anasema jumla ya majiko banifu 595 yametengenezwa katika vijiji vinavyotekeleza mradi huu (Melela 170, Lubungo 137, Mingo 141 na Magali 147 kati ya majiko 460 yaliyokuwa yanatarajiwa kujengwa ili kupunguza msukumo wa matumizi ya misitu kwa nishati ya kuni.

Anabainisha kuwa jumla ya miti 86,479 inaendelea kutunzwa katika mashamba ya wananchi wa vijiji hivyo.

"Kwenye eneo hilo mradi umekwishawezesha vikundi kadhaa vya ufugaji wa nyuki- Lubungo, utengenezaji wa sabuni na uzalishaji wa uyoga. Mpaka sasa jumla wanavikundi 78 wananufaika na miradi hii," anasema.

# Wadaiwa kuua wake zao, mmoja anywa sumu baada ya kuua

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

MKE na mume wamefariki dunia na kuacha mtoto mwenye umri wa miezi miwili baada ya mume kudaiwa kumuua mke wake ambaye alikuwa mwalimu wa shule ya msingi kisha kunywa sumu kwa kinachodaiwa wivu wa kimapenzi.

Mwanamume huyo aliyekuwa mfanyabiashara, mkazi wa Kijiji cha Amani wilayani Namtumbo, Mtolela Hashimu, anadaiwa kutekeleza mauaji hayo usiku wa kuamkia Januari 11 mwaka huu.

Mchungaji wa Kanisa la Biblia kijijini hapo, Isaya Obeid, alidai kuwa asubuhi ya Januari 11 alifika nyumbani kwa marehemu kwenda kubadilisha mbegu ya mahindi na kukuta mlango wa nyumba ukiwa wazi, alipoita hakujibiwa, lakini alisikia sauti ya mtu kukoroma hali iliyomshtua.

Alisema aliamua kwenda nyumba ya jirani yake, Selemani Kitambi kumweleza alichokisikia na wote wawili walikwenda kwenye nyumba hiyo na kuendelea kusikia sauti ya kukoroma.

Aliendelea kusimulia kuwa waliamua kwenda kutoa ripoti Ofisi ya Mtendaji wa kijiji. Wajumbe wa serikali ya kijiji walifika kwenye nyumba hiyo, walipoingia ndani walimkuta Hashimu akigalagala chini akiwa taabani na kuamua kumkimbiza Kituo cha Afya Lusewa ambako walitakiwa kumpeleka Hospitali ya Mkoa Songea. Hata hivyo, usiku wa kuamkia Januari 12, alifariki dunia akiwa hospitalini hapo.

Mchungaji huyo alisema wakati wakimhangaikia Hashimu, kitandani kulikuwa na mwili wa mke ambaye inadaiwa aliuawa na mumewe na mwili wake kufunikwa vizuri.

Alisema wajumbe wa serikali ya kijiji walimuomba muuguzi wa Zahanati ya Amani aliyekuwa eneo la tukio kuuangalia mwili huo na kuthibitisha kuwa alishafariki dunia.

Ofisa Elimu Msingi wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo, Juma Fulluge, alisema wamepokea taarifa hiyo ya kuuawa kwa mwalimu huyo.

Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Ruvuma, ACP Marco Chillya, alithibitisha kutokea kwa vifo hivyo na kwamba chanzo ni wivu wa kimapenzi.

Katika tukio lingine, Joyce Masanja, mkazi wa Ngokolo, Manispaa ya Shinyanga anadaiwa kuuawa na mume wake, Thomas Mathias kwa kuchomwa kisu sehemu mbalimbali za mwili wake kisha kutupwa jirani na msikiti wa Binti Haji mjini hapa.

Tukio hilo lilitokea juzi majira ya saa sita usiku kwenye Mtaa wa Kalonga, Kata ya Ngokolo, Manispaa ya Shinyanga.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Kalonga, Victor Ochieng, akisimuliza tukio hilo, alisema wanandoa hao walikuwa na ugomvi uliotokana na wivu wa mapenzi na wakati wakiendelea kupigana, mwanamume anadaiwa kuchukua kisu na kuanza kumchoma sehemu mbalimbali za mwili mke wake na kusababisha mauaji.

"Ugomvi wa wanandoa hawa ulianza majira ya saa sita usiku kwa mujibu wa taarifa ambazo nilizipata, na kulipokucha asubuhi tumeukuta mwili wa mwanamke umetupwa hapa jirani na msikiti wa Binti Haji Ngokolo," alidai Ochieng.

Alisema kuwa baada ya kutokea mauaji hayo, alitoa taarifa kwa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga ambalo askari wake walifika eneo la tukio na kuuchukua mwili.

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Janeth Magomi alithibitisha kutokea kwa tukio hilo la mauaji na kubainisha kuwa wanamshikilia mume wa marehemu.

Alisema chanzo cha mauaji hayo ni wivu wa mapenzi, akifafanua kuwa mwanaume alikuwa akimtuhumu mke wake kuwa na uhusiano na mwanamume mwingine.

***Imeandaliwa na Gideon Mwakanosya (SONGEA) na Marco Maduhu (SHINYANGA)**



## Aweso awashukia watendaji chanzo ukosefu wa maji

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso amewanyooshea kidole watendaji wa serikali walioshindwa kudhibiti shughuli za binadamu zinazosababisha kukosekana kwa maji katika Jiji la Tanga, kunakosababishwa pia na uchafuzi wa chanzo cha maji katika Bwawa la Mabayani.

Kutokana na tatizo hilo, Aweso alilazimika kuwaomba radhi wakazi wa jiji hilo na viunga vyake, huku akiielekeza Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jijini Tanga (Tanga-UWASA) kutekeleza majukumu yao bila kusukumwa, huku pia akiwataka kuhakikisha tatizo hilo halijirudii.

Waziri Aweso alitoa maelekezo hayo jana alipotembelea chanzo hicho pamoja na mtambo wa kusafisha maji uliopo Mowe, kujionea hali ya maji ambayo amedai hayako katika hali ya kawaida kutokana na kuchafuliwa na shughuli za binadamu.

Alisema: "Baada ya kupata taarifa kwa viongozi Jiji, nimefika kutembelea chanzo cha maji, watu wote katika jiji la Tanga hutegemea maji kutoka Mto Zigi na kwa hali niliyoikuta hapa, maji yamechafuka kutokana na shughuli zinazofanyika.

Aliongeza: "Nimeagiza wataalamu wa mtambo wa maji wa Mowe, kuyatibu na kuyasafisha maji hayo kabla ya kuyaruhusu kwenda kwa wananchi. Hata hivyo nimetoa maelezo kwamba wakiona maji yanayokwenda yamebadilika, wazime mitambo kwa muda lakini watoe taarifa kabla kwa wananchi.

Alisema: "Lakini hili la kukosekana kwa maji, ndiyo kelele za wananchi zikaanza kuleta taharuki, na ndiyo maana serikali ipo hapa na wale wataalamu wameanza kuyatibu na sasa yako safi na salama. Kwa dhati ya moyo wangu nawaomba radhi kwa jambo hili lililojitokeza."

Akiwa Tanga Mjini, Waziri Aweso, pia alitembelea baadhi ya makazi ya wananchi kwenye Kata za Chumbageni na Ngamiani Kusini na kushuhudia huduma yam aji ikirejea. Mkurugenzi Mtendaji wa Tanga-UWASA, Geoffrey Hilly, alisema taarifa iliyowafilia wananchi ya kuchafuka kwa maji, iliwashtua kwa kuwa haikuwa ile ya kawaida ya kukosekana kwa umeme kama walivyozoea.

# Wapinga operesheni upimaji ardhi kisa kutoshirikishwa

**Cynthia Mwilolezi na Allan Isaack,** NGORONGORO

WANANCHI 4,000 wa Kijiji cha Kisangiro kilichoko Kata ya Kirangi, Wilaya ya Ngorongoro, mkoani Arusha, wamepinga operesheni ya upimaji wa ardhi iliyofanywa na idara ya ardhi wilayani humo, wakidai kutopewa elimu wala kushirikishwa.

Kutokana na sakata hilo, wamemuomba Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kuingilia kati suala hilo ili wapate haki ya kubaki katika eneo lao lenye ukubwa wa hekta 7,558.4, waweze kuendesha shughuli zao za kilimo.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji hicho, Michael Samawa, alisema baada ya upimaji huo kufanyika ardhi yao imehamishiwa Kijiji cha Enguserosambu, hivyo kukwamisha kuendelea na shughuli za kilimo.

"Wanakisangiro tuna kilio kikubwa sana ambacho kimeleta hatari ndani ya kijiji chetu ni vijana wengi wamepotea kwa ajili ya ardhi hii, kutokana wananchi wa kijiji jirani kukumbatiwa na baadhi ya viongozi wa Wilaya ya Ngorongoro kwa kuwahalalishia eneo letu la kitongoji kizima hata bila kutushirikisha wenyeji,"alisema Mwenyekiti Samawa.

Alisema ramani ya mipaka yao awali inaonyesha inapoishia, lakini cha kushangaza eneo hilo viongozi hao wameenda kuwapa Kijiji cha Enguserosambu, hali ambayo inadhihirisha rushwa kwa sababu wameshapeleka malalamiko yao lakini hayafanyiwi kazi.

Samawa alisema Aprili 23 mwaka huu aliyekuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Prof. Anna Tibaijuka, alikwenda Wilaya ya Ngorongoro kutatua migogoro ya ardhi ikiwamo Kisangiro na Enguserosambu, ambapo alijidhihirisha na mipaka ya maeneo yao na kuruhusu itumike, lakini cha kushangaza watendaji wa wilaya hiyo wamekiuka.

Akizungumzia sakata hilo, Diwani wa Kirangi, Phillipo Moloi, alisema jamii ya wakazi wa Kisangiro hadi sasa haijapata utulivu kutokana na eneo lao kubwa kumegwa na kurudishwa kijiji jirani, hali inayovunja amani.

"Timu ya upimaji haijatenda haki kwani viongozi wa kijiji walisimama kuhakikisha haki inapatikana, lakini hawakusikilizwa na hadi sasa hivi Mwenyekiti wa Kijiji hajasaini kutokana na kutokukubaliana kwa kile kilichofanyika,"alisema Moloi.

Alipoulizwa Mkuu wa Wilaya ya Ngorongoro, Raymond Mangwala kuhusu sakata hilo, alisema katika operesheni hiyo ya upimaji wa ardhi, wameshapima vijiji 36, lakini yapo maeneo yenye malalamiko ambayo wameyapokea na wanaendelea kuyafanyia kazi.

Mangwala alisema ili kijiji kiweze kupimwa ni lazima kamati zikutane na wataalamu wa upimaji wa ardhi ngazi ya wilaya, lakini maeneo mengine yalikuwa yanapata changamoto ya baadhi ya viongozi kijiji kukimbia zoezi hilo, ambalo lilitakiwa likamilike kwa wakati uliopangwa.



Mkuu wa Wilaya ya Lushoto mkoani Tanga, Kalist Lazaro (Wapili kulia) akiwa na viongozi wenzake katika ziara ya kutembelea kata za Dule na Mwangoi kukagua ujenzi wa daraja lililopo eneo la Mlesa pamoja na barabara ya Majulai-Mlesa. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Waziri: Hakuna mwanafunzi kuvuka darasa kama hajui KKK

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angela Kairuki, ameagiza maofisa elimu ngazi zote na walimu wa wakuu wa shule za msingi kuhakikisha wanafunzi wa darasa la kwanza hawavuki darasa hilo kabla ya kujua kusoma, kuandika na kuhesabu.

Aidha, ameagiza maofisa elimu ya msingi nchini kuruhusu mchakato wa uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la awali uliokuwa umewekewa ukomo wake Desemba 31 mwaka jana, unaendelea tena kwa mwezi huu.

Kairuki alitoa maelekezo hayo mwishoni mwa wiki, wakati wa kikao cha mapitio ya tathimini ya utekelezaji wa shughuli za uboreshaji na usimamizi wa elimu nchini.

Katika kikao hicho hotuba ya Kairuki ilisomwa na Mkuu wa Mkoa huo, Makongoro Nyerere.

"Bado kuna wanafunzi wanamaliza darasa la kwanza bila kujua kusoma, kuandika na kuhesabu. Kuanzia mwaka huu, tunataka wanafunzi wote wanapotoka darasa la kwanza kwenda darasa la pili, wawe na ustadi wa kujua kusoma, kuandika na kuhesabu na sio kuwapitisha tu.

"Kila mwalimu ajiwekee malengo binafsi ya kuhakikisha wanafunzi wanahudhuria shuleni, kuwepo chakula cha mchana na kiwepo kipimo kwa walimu na maofisa elimu. Viongozi waendelee kuendelea kuhakikisha wanafunzi wa elimu ya awali na kufikia malengo mliojiwekea kuandikisha wanafunzi."alisema.


Katibu Mkuu wa TAMISEMI, Dk. Charles Msonde, akizungumza katika kikao hicho kuhusu uwezo mdogo wa wanafunzi wa darasa la awali na la kwanza, alisema haiwezekani mwanafunzi wa darasa la awali au darasa la kwanza, amalize mwaka hajui kitu chochote, kwa kuwa walimu wamepewa maelekezo ya kuwaandaa ili kufikia malengo ya kitaaluma.

Dk. Msonde alisema: "Ofisa Elimu Mkoa, ukiona kuna wasaidizi wako wa ngazi za chini wanakukwamisha tuambie tuwale kichwa, wasiendelee kukwamisha utendaji wa kazi. Vilevile, kuanzia sasa hakuna maofisa elimu kukaa ofisini muda wote, ondokeni nendeni shuleni mkasikile walimu na kutatua kero zao,"alisema Dk. Msonde.

Alisema kitu kinachoshangaza ni kuwapo kwa wanafunzi wanaotoka darasa la kwanza hawajui kusoma, kuandika na kuhesabu na kusababisha ugonjwa huo kwenda nao mpaka darasa la nne.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Manyara (RAS), Karoline Mthapula, akiwasilisha taarifa ya elimu ya mkoa huo alisema shule za msingi 503 pekee ndizo zinazotoa chakula cha mchana kati ya 600.

Mratibu wa Elimu Kata ya Garawja, Athuman Kangile, alisema suala la KKK (kusoma, kuandika na kuhesabu), linawezekana kwa sababu huenda walimu walikuwa wamekata tamaa, ila sasa watabadilika.







Mbunge wa jimbo la Ushetu wilayani Kahama mkoani Shinyanga, Emmanuel Cherehani, akizungumza na wananchi wa kijiji cha Butibu kata ya Kinamapula wakati wa ziara yake ya ukaguzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo jana, **PICHA: SHABAN NJIA.**

# Wananchi wahofia usalama wahalifu kuachiwa bila kufikishwa kortini

**Na Richard Makore,** SERENGETI

HALI ya usalama katika mpaka wa vijiji vya Remng'orori wilayani Serengeti na Mekamariro, wilayani Bunda imezidi kuwa tete baada Jeshi la Polisi kukamata wahalifu saba wakiwamo wanaodaiwa kuhusika na mauaji, wizi wa mifugo na kubomoa nyumba za watu kisha kuachiwa bila kuwafikisha mahakamani.

Watu hao walikamatwa hivi karibuni na kushikiliwa kwa siku sita wilayani Serengeti na kisha kuachiwa kwa madai kuwa ni agizo kutoka ngazi ya juu.

Akizungumza na Nipashe, Mkuu wa Jeshi la Polisi wilayani Serengeti, Mathew Mgema, alikiri watu hao kukamatwa mpakani mwa vijiji hivyo na mmoja wapo wa wahalifu hao akiwa na bunduki aina ya gobore.

Alisema wahalifu hao wanaongozwa na mtu aliyemtaja kwa jina la Maghera Nyamhanga ambao wamekuwa wakifanya uhalifu katika kijiji cha Remung'orori wilayani Serengeti.

Hata hivyo, alisema baada ya watu hao wanaodaiwa kufanya uhalifu yakiwamo mauaji ya watu wawili mwaka 2018, kulikuwa na shinikizo la kutaka waachiwe.

Kutokana na shinikizo hilo, Alhamisi wiki iliyopita waliachiwa bila kufikishwa mahakamani, hatua ambayo imezidi kuleta hofu katika eneo hilo ambalo pia limekuwa na mgogoro wa muda mrefu kugombea ardhi.

"Watu hawa tuliwakamata wakiwa na silaha za jadi pamoja na bunduki, lakini 'presha' ni kubwa nataka niwapeleke huko Musoma wenyewe wawaachie," alisema.

Akizungumza na Nipashe, Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Mara, Longinus Tibishibwanu, alikiri watu hao kukamatwa na kushikiliwa na polisi.

Alisema aliagiza ifanyike operesheni kuwasaka watu hao kwa kuwa wamekuwa wakifanya uhalifu kwa kisingizio cha kugombea ardhi.

"Ni kweli tumewakamata watu hao na tutawafikisha kwenye vyombo vya sheria ili kukomesha uhalifu unaofanywa na watu kutoka kijiji cha Mekomariro wilayani Bunda wanaoingia wilayani Serengeti," alisema.

Kuhusu wahalifu hao kutetewa na watu walio na mamlaka, alisema hakuna mtu anaweza kulinda mhalifu katika eneo lolote.

Awali, Mwenyekiti wa kijiji cha Remung'orori, wilayani Serengeti, Msamba King'anyi akizungumza na Nipashe alisema wahalifu hao wamesababisha wananchi wake kushindwa kufanya shughuli za kilimo na ufugaji.

Alisema kwa sasa wanaishi kwa hofu na kila mara wakitoa taarifa polisi hakuna hatua zinazochukuliwa.

Aliongeza kuwa wahalifu hao wanajulikana, lakini kumekuwa na ugumu wa kuwadhibiti mpaka kusababisha uharibifu yakiwamo mauaji, wizi wa mifugo pamoja na uvamizi wa mashamba.

Alimuomba Mkuu wa Jeshi la Polisi Nchini (IGP), Camilius Wambura, kuingilia kati ili watu hao wakamatwe na kufikishwa mahakamani.

King'anyi alisema kwa muda mrefu amekuwa akiwasihi wananchi wake kutii sheria, lakini anaona uvumilivu utafika mwisho kwa kuwa polisi wameshindwa kudhibiti uhalifu huo ambao unafanyika mchana.

Alisema ikiwa hali ikiendelea kuwa hivyo kunaweza kutokea mapigano ya wananchi wa vijiji hivyo viwili.

# RC aagiza wazazi wasiopeleka watoto shule kukamatwa

**Elizabert Seleman,** SENGEREMA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Adam Malima, ameagiza kukamatwa wazazi na walezi wa wanafunzi zaidi ya 8,000 walioshindwa kuwapeleka wanafunzi shule waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka huu.

Malima alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki wakati akipokea vyumba 152 vya madarasa katika Shule ya Sekondari ya Nyampulukano, katika Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema, mkoani Mwanza.

Alisema ikifika keshokutwa wazazi na walezi wahakikishe wanawapeleka watoto kuripoti shuleni kwa ajili ya kuanza masomo yao ya kidato cha kwanza, vinginevyo watakamatwa na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria.

Akipokea vyumba vya madarasa Malima aliitaka shule hiyo kuitunza miundombinu hiyo ya madarasa ili iweze kudumu.

Mkuu wa Wilaya ya Sengerema, Senyi Ngaga, akikabidhi madarasa hayo kwa Mkuu wa mkoa, alisema hataki kuona wala kusikia mzazi au mlezi hajampeleka mtoto shuleni.

Alisema wazazi wote wanatakiwa kuwapeleka wanafunzi shuleni na sio kuwaacha nyumbani kwa kisingizio cha kukosa fedha za kuwanunulia mahitaji. Aidha, Ngaga alisema wanafunzi wanatakiwa kuripoti shuleni huku wakiendelea kufanya maandalizi ya sare za shule.

Akisoma taarifa kuhusu ujenzi wa madarasa hayo, Mkurugezi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema, Binuru Shekidele, alisema ana jumla ya wanafunzi 27,000 na uhitaji ni vyumba vya madarasa 604 na kwa sasa vilivyopo ni 210.

Aliomba serikali kuongeza madarasa ili kukidhi mahitaji ya sasa.

Alisema idadi ya vyumba vya madarasa ambavyo vimejengwa na kukabidhiwa ni 152.

# Ubovu barabara walazimisha wajawazito kubebwa machela

**Na Elizabeth Seleman,**

SENGEREMA

WAJAWAZITO wa vijiji vya Shimaka na Nyanzumla, wilayani Sengerema wanalazimika kubebwa kwenye machela wanapokwenda kujifungua kituo cha afya kilichopo kata ya Kaguga kutokana na ubovu wa barabara.

Waizungumza na Nipashe katika ziara ya Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wilayani Sengerema, Jackson Mazinzi, wananchi wa vijiji hivyo hivyo walisema wanakabiliwa na ubovu wa miundombinu ya barabara.

Mmoja wa wananchi hao, Amosi Katumbi mkazi wa Kata ya Kaguga, aliomba serikali iwasaidie kutatua tatizo hilo.

Alisema ubovu wa barabara unasababisha wananchi kukosa huduma na mahitaji muhimu yakiwamo ya afya.

Akizungumza na Nipashe, Debora Simon kutoka kiijiji cha Nyanzumla, alisema inawalazimu wanawake wa kijiji hicho kubebwa kwenye machela wanapoenda kujifungua na muda mwingine kujingufulia njiani kutokana na ubovu wa barabara.

Wananchi hao walisema ni kipindi kirefu wanakabiliwa na tatizo hilo la ubovu wa barabara licha ya wenyewe kujitolea kusomba mawe kwa ajili ya kutengeneza karavati, lakini bado hawajapata msaada wowote.

Diwani wa Kata ya Kaguga, Michael Masuga, alisema wapo kwenye mchakato wa kutengeneza barabara ambazo ni mbovu katika kata hiyo na kuwaomba wananchi wawe wavumilivu wakati serikali inapoendelea na matengenezo.


Aidha, alisema Wakala wa Barabara za Mjini na Vijijini (TARURA), wilayani Sengerema imepitisha bajeti ya Sh. bilioni 2.2 kwa mwaka wa 2023/2024 kutengeneza barabara mbovu.

Nipashe
# Spotika



WAZENJI WA5 WALIOBEBWA NA KOMBE LA MAPINDUZI UK. 14




# REKODI 3 ZA RONALDO AMBAZO MESSI SASA ANAWEZA KUZIVUNJA

## ISIKUPITE

Jezi ambayo Lionel Messi alivaa katika mchezo wake wa kwanza akiwa na Paris Saint-Germain (PSG) baada ya Kombe la Dunia la FIFA 2022 imepokea ofa ya Euro 20,000 katika mnada uliofanyika kwenye MatchWornShirt.com. Jezi hiyo aliyovaa Messi imeandikwa "GOAT" kwenye mkono wa kushoto na kampuni hiyo inayoifadhili PSG. Mnada unaendelea na bei ya jezi hiyo bado inaweza kupanda. Messi alirejea uwanjani akiwa na klabu yake wakati wa mechi ya Ligue 1 dhidi ya Angers, ambayo PSG ilishinda 2-0.




**PARIS,** Ufaransa

BAADA ya Cristiano Ronaldo kuhamia Al Nassr, Lionel Messi ana nafasi ya kuvunja rekodi tatu za nyota huyo wa kimataifa wa Ureno barani Ulaya.

Messi na Ronaldo wamekuwa kwenye vita vya kuwania ukuu kwa takriban miongo miwili. Mastaa hao wawili wamesukumana kupita mipaka yao na wamevunja rekodi kadhaa katika mchakato huo. Wakubwa wawili wa kizazi hiki sasa wanashikilia rekodi nyingi za soka kwa majina yao, na hakuna mchezaji aliyekaribia.

Hata hivyo, Ronaldo hatacheza tena Ulaya, na kumwacha Messi katika Klabu ya Paris Saint-Germain akiwa na nafasi ya kukamata na kuzipita baadhi ya rekodi za Ronaldo katika siku za usoni. Sasa tuangalie rekodi tatu ambazo anaweza kuvunja...

**#1. Mabao mengi zaidi Ligi za Ulaya**

Ronaldo alimpita Messi na kuwa mwanasoka aliyefunga mabao mengi zaidi katika ligi tano bora barani Ulaya. Mreno huyo alifunga mabao 696 wakati akiwa na Manchester United kwenye Ligi Kuu, Real Madrid kwenye La Liga, na Juventus kwenye Serie A.

Aliruka mbele ya Muargentina huyo katika msimu ya hivi karibuni baada ya nyota huyo wa PSG kudorora kwa kiwango chake. Hata hivyo, mshindi huyo wa Kombe la Dunia la FIFA yuko nyuma kwa bao moja tu na anaweza kumpita nyota huyo wa Ureno ikiwa atapata bao mara mbili kwenye Ligue 1.

Ikiwa Messi akifunga mara mbili katika mchezo unaofuata anaocheza kwenye Ligi ya Ufaransa, atafanya hivyo katika mechi 832, huku Ronaldo alihitaji mechi 919.

**#2. Asisti nyingi Uefa**

Mashabiki mara nyingi huhusisha Messi na pasi za mabao uwanjani ikilinganishwa na Ronaldo, lakini sivyo ilivyo katika Ligi ya Mabingwa Ulaya. Nyota huyo wa zamani wa Real Madrid ametoa pasi 41 za mabao kwenye michuano hiyo, huku nyota wa PSG akiwa na 40.

Huku Ronaldo akienda kucheza Ligi ya Saudi Arabia, Messi ana nafasi ya kumpita nyota huyo wa Ureno mwaka huu. PSG itamenyana na Bayern Munich katika hatua ya 16-bora, na Muargentina huyo anahitaji pasi mbili pekee za mabao ili kuwa mchezaji mwenye asisti nyingi zaidi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

**#3. Mabao mengi Uefa**

Messi atakuwa na wakati mgumu kushinda idadi ya mabao ya Ronaldo kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35, anatakiwa kufunga mabao 12 zaidi ili kumpita nyota huyo wa Ureno, na kwa awamu ya mtoano kuanza, itamlazimu aende kwa kasi ya ajabu kufika huko.

Hata hivyo, Messi anatarajiwa kusaini mkataba mpya katika Klabu ya PSG au uwezekano wa kurejea Barcelona msimu ujao, ambao hatimaye utamhakikishia nafasi yake ya kushiriki michuano ya Ulaya kwa msimu mwingine.

Wafaransa wapo kileleni mwa Ligue 1 na wanatajwa kutwaa ubingwa huo, huku timu hiyo ya Katalunya ikifanya vema. Timu zote mbili zinatarajiwa kushuhudia tena Ligi ya Mabingwa Ulaya mwakani. Messi anaweza kuvunja rekodi ya Ronaldo kwa urahisi akipewa misimu miwili kuifanikisha, ikiwa si zaidi.

## Extra Time

# WACHEZAJI WA5 'VIRAKA' DIMBANI



JOAO CANCELO

**LONDON,** England

WACHEZAJI hodari huunda uti wa mgongo wa timu. Hawatoi tu kwa kocha wao kubadilika kwa majaribio na mifumo tofauti, lakini pia hujaza nafasi za wachezaji wenzao waliojeruhiwa inapohitajika. Uwezo wa kucheza katika nafasi nyingi (kiraka) ni mojawapo ya sifa kuu ambazo mchezaji anaweza kuwa nazo.

Leo, tutaangalia wachezaji wachache ambao wamekuwa kivutio cha kocha wao, wakitoa uchezaji wa kuvutia bila kujali nafasi wanayopelekwa. Hapa chini kuna wanasoka watano wenye uwezo wa kucheza nafasi nyingi zaidi duniani kwa sasa...

**#5. Danilo Pereira - Paris Saint-Germain**

Danilo Pereira hawezi kuwa na nafasi mbele ya baadhi ya nyota wa kimataifa wa Paris Saint-Germain walio nao. Lakini linapokuja suala la matumizi mengi, hakuna mtu bora zaidi kwenye klabu hiyo kuliko Mreno huyo.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno kwa kiasi kikubwa ni kiungo mkabaji, lakini si nafasi pekee anayoweza kuicheza kwa ufasaha. Pereira amejidhihirisha kuwa beki wa kati wa kutegemewa msimu huu, na kuisaidia timu yake kupata matokeo muhimu wakati Presnel Kimpembe alipokuwa majeruhi. Pereira alikuwa imara upande wa kushoto wa safu ya nyuma ya wachezaji watatu wa kocha Galtier, mara chache aliweka mguu vibaya katika mechi 10 alizocheza kwenye nafasi hiyo.

Pereira, ambaye alirejea mazoezini hivi karibuni baada ya kupona jeraha la mbavu, amecheza mechi 18 akiwa na PSG msimu huu, akifunga mara moja.

**#4. Joao Cancelo - Manchester City**

Anayetajwa sana kuwa mmoja wa mabeki bora zaidi duniani, nyota wa Manchester City, Joao Cancelo, ni beki mmoja hodari sana. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno anayetumia mguu wa kulia kwa kawaida ni beki wa kulia, lakini ana uwezo sawa na upande wa pili pia.

Cancelo ana kasi nyingi, anajua jinsi ya kupanga wachezaji wenzake, na huweka uwiano mzuri kati ya mashambulizi na ulinzi. Yeye ni mmoja wa walinzi wachache sana duniani wenye uwezo wa kushambulia ambao hawapuuzi majukumu yao ya ulinzi kwa kurudi nyuma haraka.

Kwa nyongeza, Cancelo ni mzuri katika mipira ya juu. Supastaa huyo wa Ureno amefanikiwa kuwa kiungo wa kulia na winga katika mfumo wa 3-2-4-1 msimu huu, akiweka krosi hatari mara kwa mara kwenye eneo hatari. Mchezaji mahiri zaidi wa City, Cancelo ameichezea klabu hiyo mechi 24 msimu huu, akifunga mara mbili na kutoa pasi tatu za mabao kwenye mashindano yote.

**#3. David Alaba - Real Madrid**

Wengi walishangaa wakati Real Madrid ilipomsajili David Alaba kabla ya msimu wa 2021-22. Na Sergio Ramos akiwa bado kwenye timu, nyongeza ya Muaustria huyo haikuwa na maana sana. Na Ramos aliondoka kwenda PSG muda mfupi baadaye, na kumpa Alaba fursa ya kuwa chaguo la kwanza kwenye timu.

Beki huyo mahiri, ambaye aliwahi kuwa beki wa kushoto kwa muda mwingi wa uchezaji wake kule Bayern Munich, alichukua jezi namba nne ya Ramos. Alaba aliibuka kama mmoja wa wachezaji bora wa Real Madrid msimu wa 2021-22 waliposhinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, Ligi Kuu Hispania, LaLiga, na Spanish Supercup.

'Los Blancos' walimsajili Antonio Rudiger msimu uliopita wa majira ya joto, lakini Alaba amebakia kuwa mmoja wapo wa majina ya kwanza kwenye orodha ya kikosi cha kwanza cha timu hiyo, na kwa sababu nzuri tu. Sio tu kwamba yeye ni beki bora wa kati, lakini pia ana uwezo wa kucheza kiungo mkabaji na mshambuliaji. Pia ana uwezo wa kusukuma mashambulizi mbele na kutoa krosi za mabao.

Tangu kuanza kwa msimu huu, Alaba amecheza mechi 22 katika mashindano yote, akifunga mara mbili na kutoa pasi tatu za mabao.

**#2. James Milner - Liverpool**

Nyota wa Liverpool, James Milner ndiye mchezaji mahiri zaidi katika Ligi Kuu England. Tabia ya Milner kubadilika imemsaidia Jurgen Klopp kudumisha akili timamu wakati wa majeraha, na Muingereza huyo huwa na nafasi ya kuchukua jukumu la kucheza nafasi nyingine.

Awali, alikuwa akicheza kama kiungo wa kati, lakini pia ana uwezo wa kucheza upande wa kushoto au kulia kwa safu ya kiungo. Ikiwa hiyo haikuwa ya kuvutia vya kutosha, Milner amethibitisha kuwa mchezaji wa pembeni. Katika msimu wa 2016-17, Milner aliwahi kuwa chaguo la kwanza la beki wa kushoto wa Liverpool.

Msimu huu, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 37 amekuwa akicheza nafasi ya kiungo wa kati. Ameshiriki katika michezo 20 kwa klabu hiyo ya Merseyside katika mashindano yote, akitoa asisti mbili.

**#1. Federico Valverde - Real Madrid**

Real Madrid hawana uhaba wa wachezaji mahiri, lakini Federico Valverde labda ndiye mchezaji mwenye bidii zaidi. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uruguay, kiasili ni kiungo wa kati, lakini uwezo wake wa kusoma mchezo, ukakamavu, na maono humruhusu kushiriki katika nafasi yoyote.

Katika kipindi cha pili cha msimu wa 2021-22, kocha wa Real Madrid, Carlo Ancelotti, kimsingi alimtumia mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, kama winga wa kulia. Shukrani kwa kasi na stamina yake, alionekana kuwa mtu wa kawaida katika jukumu hilo, akiisaidia klabu hiyo kushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya, LaLiga na Supercup.

Msimu huu, amecheza hasa katika safu ya kiungo pamoja na Toni Kroos au Luka Modric, lakini pia amenyoosha miguu yake chini upande wa kulia.

Valverde ameichezea 'Los Blancos' katika michezo 28 msimu wa 2022-23, akiwa amefunga mabao nane na kutoa pasi nne za mwisho.

## Nukuu

"Sijui siku zijazo, lakini nina furaha sana Real Madrid. Niko ndani ya mkataba hadi 2024 na wasiponifukuza, sitaondoka. Kutakuwa na wakati wa kufikiria juu ya maisha yangu ya baadaye," **Kocha wa Real Madrid, Carlo Ancelotti, akifafanua kuhusu kuhusishwa kazi ya kuinoa Timu ya Taifa ya Brazil.**



"Kuna wakati unapovuka, na unakasirika. Lakini jukumu langu ni kuzungumza (na vyombo vya habari) kwa heshima niwezavyo, ingawa baadhi ya maswali yako ni ya kijinga. Lazima niwajibu kadri niwezavyo na kwa heshima niwezavyo, kwa sababu ninawakilisha klabu nzuri ya soka, na nina kazi hiyo ya kufanya," **Kocha Mkuu wa Chelsea, Graham Potter, akizungumza na vyombo vya habari baada ya 'Blues' hao kupata ushindi mara moja katika mechi nane za Ligi Kuu, ikiwa ni baada ya kupoteza kwa mabao 4-0 kwenye FA Cup dhidi ya Manchester City.**



"Maamuzi ya soka lazima yafanyike uwanjani, mimi si kocha mwenye maamuzi ya ofisini, kwa hiyo mimi pa kuanzia ni kuwafikia wachezaji wote na nataka niwasiliane nao. Orodha ya wachezaji 26 kutoka Kombe la Dunia ndio hatua yangu ya kuanzia na Cristiano ni mchezaji kwenye orodha hiyo, amekuwa na timu ya taifa kwa miaka 19 na anastahili heshima ya kuweza kukaa chini na kuzungumza," **Roberto Martinez alizungumza kuhusu mipango yake kwa Ronaldo, baada ya kupewa jukumu la kuinoa Timu ya Taifa ya Ureno.**



"Kuna wakati unapovuka, na unakasirika. Lakini jukumu langu ni kuzungumza (na vyombo vya habari) kwa heshima niwezavyo, ingawa baadhi ya maswali yako ni ya kijinga. Lazima niwajibu kadri niwezavyo na kwa heshima niwezavyo, kwa sababu ninawakilisha klabu nzuri ya soka, na nina kazi hiyo ya kufanya," **Kocha Mkuu wa Chelsea, Graham Potter, akizungumza na vyombo vya habari baada ya 'Blues' hao kupata ushindi mara moja katika mechi nane za Ligi Kuu, ikiwa ni baada ya kupoteza kwa mabao 4-0 kwenye FA Cup dhidi ya Manchester City.**

Uk. 12-13

# WAZENJI WA5 WALIOBEBWA NA KOMBE LA MAPINDUZI

**Na Adam Fungamwango**

MLANDEGE ya Zanzibar ilitwaa Kombe la Mapinduzi Ijumaa iliyopita baada ya kuichapa Singida Big Stars na kuhitimisha ukame wa miaka 13 kwa timu za hapo kutwaa ubingwa huo.

Mlandege ilipitia njia ngumu hadi kutwaa kombe hilo, ikiwa Kundi C ikiichapa Simba bao 1-0, na mechi ya nusu fainali ikaitoa Namungo kwa mkwaju 5-4 ya penalti, kabla ya kushinda mabao 2-1 kwenye mchezo wa fainali.

Hata hivyo, pamoja na kutotwaa ubingwa kwa miaka yote hiyo, lakini Kombe la Mapuduzi huwa kama jukwaa la wachezaji wa Kizanzibari kuonekana na klabu mbalimbali, husan za Tanzania Bara.

Na msimu huu timu nyingi za Zenji zimefanya vizuri sana na wala haikuwashangza mashabiki wengi kuona moja ya timu za huko ikitwaa ubingwa. Kama kawaida ya miaka yote, baadhi ya wachezaji wameshaanza kuonekana na kuvutia klabu mbalimbali Bara.

Straika wa Mlandege, Bashima Sauli Saite, ameweka wazi kuwa ameshaanza kupokea simu kutoka Tanzania Bara zikihitaji huduma yake.

Straika huyo mwenye mwili uliojengeka kimichezo na aliyewasumbua sana mabeki wa Singida Big Stars, ameweka wazi kuwa kama si kipindi hiki cha dirisha dogo, basi msimu ujao ataonekana Bara.

Golikipa wa Mlandege, Yusuph Abdul Ally, aliyeonyesha uwezo mkubwa tangu kuanza kwa michuano hiyo na kuwa kipa bora wa mashindano, alisema mpira ni kazi yake, na tayari simu zimeshaanza kumiminika.

Katika makala haya tutawaangalia baadhi ya wachezaji waliowika kwenye michuano ya Kombe la Mapinduzi na kupata timu Bara, twende sasa...

**#1. Ibrahim Rajab 'Jeba'**

Mwaka 2012, kulikuwa na mchezaji aliyewika kwenye Kombe la Mapinduzi akiichezea Chuoni FC. Ni Abrahim Rajab 'Jeba.' Baada ya kumalizika kwa michuano hiyo alisajiliwa Tanzania Bara na Klabu ya Azam FC, licha ya kwamba Simba nayo ilikuwa ikimhitaji.

Simba ilitaka kuifanyia umafia Azam na kumsajili ilipomsajili mchezaji huyo na kujiunga nayo kwa mazoezi, lakini hakuweza kuichezea kwa kuwekewa ngumu na Azam FC iliyokuwa tayari na mkataba naye wa miaka miwili. Baadaye aliichezea pia Mtibwa Sugar kwa kipindi kirefu. Mchezaji hiyo alifariki dunia Zanzibar mwaka 2019.



'FEI TOTO'

**#2. Feisal Salum 'Fei Toto'**

Huyu ni mchezaji maarufu zaidi kwa sasa nchini. Fei Toto kabla ya kuvuka maji na kutinga Bara alikuwa akiichezea JKU ya Zanzibar. Baada ya kufanya vizuri kwenye Kombe la Mapinduzi mwaka 2018, Klabu ya Singida United ilimsajili kwa mkataba wa miaka miwili.

Lakini kabla hajaanza kuitumikia, kiungo huyo mshambuliaji anayeichezea Zanzibar Heroes na Timu ya Taifa ya Tanzania, alipelekwa klabu ya Yanga ambayo yupo hadi leo, ingawa kwa sasa ana mgogoro wa kimkataba na klabu yake hiyo.

**#3. Ibrahim Hilika**

Mchezaji huyu amejiunga na Polisi Tanzania kipindi hiki cha dirisha dogo akitokea Mtibwa Sugar. Ibrahim Hilika, mtoto wa mchezaji wa zamani wa Zanzibar, Hamad Hilika, naye alionekana kwenye michuano ya Kombe la Mapinduzi mwaka 2018 na akawa mfungazaji bora akiwa na timu ya Zimamoto.

Msimu uliofuata Mtibwa wakaenda kumsajili baada ya kuona amekuwa na mwendelezo kutokana na kuwa mfungaji bora wa Ligi Kuu Zanzibar 2019/20, hivyo Agosti 2020 akasajiliwa na klabu hiyo kabla ya kuihama kipindi hiki cha dirisha dogo.

**#4. Hussein Abel Thomas**

Ni mmoja wa magolikipa hodari kwa sasa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara. Alisajiliwa na Prisons kipindi cha dirisha dogo la usajili msimu uliopita.

Prisons ilimnyakuwa baada ya kuonyesha kazi nzuri na kushangaza wengi kwenye Kombe la Mapinduzi mwaka jana akiwa na kikosi cha Taifa Jang'ombe na hadi leo si tu kipa namba moja, bali Thomas Abel ni mmoja wa makipa ambao wanatajwa huenda msimu ujao asiichezea tena Prisons kutokana na kiwango chake kikubwa, kwani klabu kadhaa zimeshaanza kummezea mate.

**#5. Ibrahim Abdallah 'Bacca'**

Pamoja na kutolewa kwenye Kombe la Mapinduzi mwaka jana, Yanga haikurudi bara hivi hivi. Iliondoka na beki aliyefanya vizuri kwenye michuano hiyo akiwa na kikosi cha KMKM, Abdallah Hamad 'Bacca.'

Mchezaji huyo alipigiwa upatu mno na Nadir Haroub 'Cannavaro', ambaye naye ni mchezaji kutoka Zenji na aliichezea pia Yanga.

'Bacca' ambaye ni beki wa kati, bado yupo Yanga akiwa ni chaguo la pili kwenye kikosi hicho chini ya kocha Nasreddine Nabi.

**JE, WAJUA?**



Liverpool ndiyo klabu pekee iliyoshinda mechi nyingi zaidi (43) barani Ulaya kwa mwaka 2022, ikifuatiwa na Real Madrid (37), Manchester City (37), Paris Saint-Germain (32) na Barcelona mechi 31.



## Wizara ya Afya yaanzisha huduma ya kujipima VVU kazini

**Na Paul Mabeja,**DODOMA

WIZARA ya Afya imesema imeanzisha huduma ya kujipima Virusi Vya Ukimwi (VVU) mahala pa kazi ili kurahisisha upatikanaji wa huduma ya vipimo hivyo kwa watumishi kazini.

Imesema hadi Desemba 2022 watu wapatao 96,231 wamepatiwa huduma hiyo.

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel alibainisha hayo juzi wakati akiwasilisha taarifa kuhusu kuhuisha na kujumuisha masuala ya UKIMWI katika Kamati ya Kudumu ya Bunge ya masuala ya UKIMWI.

"Wizara imeanzisha huduma ya kujipima VVU mahala pa kazi iitwayo 'jipime' ili kurahisisha upatikanaji wa huduma ya vipimo vya VVU kwa watumishi sehemu za kazi hususani wanaume. Hadi kufikia Desemba 2022 watu wapatao 96,231 wamepatiwa huduma hiyo," alisema Dk. Mollel.

Aidha alisema hadi kufikia Desemba 2022 vijana balehe 47,705 (wavulana 20,329 na wasichana 27,376) walifikiwa katika shule 103 kupitia kampeni ya kipepeo, huku akibainisha kuwa kampeni hiyo inatarajiwa kufanyika mwaka 2023 katika mikoa ya Dodoma, Singida, Morogoro, Tanga na Geita.

Alisema mwaka 2022 Wizara ya Afya kwa kushirikiana na TACAIDS na Wizara ya Elimu imeweza kutoa mafunzo ya elimu ya jinsia kwa walimu 5,033 nchini.

Pamoja na hayo, Dk. Mollel alisema hadi kufikia Desemba 2022 kuna vituo vitano vya kutolea huduma za afya katika maeneo ya Geita Gold Mine (Geita), North Mara Gold Mine (Mara), Bulyanhulu Gold Mine Limited (Shinyanga), New Luika Gold Mine (Songwe) na Mererani (Manyara).

Alisema huduma zinazotolewa katika migodi hiyo ni pamoja na upimaji wa VVU, huduma za tiba na matunzo ikiwamo utoaji wa ARV, huduma za tohara, huduma za jipime huduma za dawa kinga na magonjwa mengine ya ngono.

Kuhusu wakazi wanaoishi maeneo yasiyifikika kwa urahisi hususani visiwani, alisema wizara imekuwa ikitoa huduma za VVU na UKIMWI kwa njia ya huduma mkoba ngazi ya jamii na baadhi ya maeneo kama visiwani hususani Ziwa Vitoria Mkoani Mwanza huduma hiyo hutolewa kwa kutumia usafiri wa boti maalum.

# TFS kupitia sheria, utaratibu utoaji leseni za ukataji miti

**Na Paul Mabeja,**DODOMA

WAKALA wa Misitu Tanzania (TFS) umesema utayafanyia kazi maagizo ya Makamu wa Rais Dk.Philip Mpango ya kupitia upya sheria na utaratibu wa utoaji leseni za ukataji miti kwa ajili ya mkaa.

Aidha, wakala huo umewataka Watanzania kulinda misitu ya asili ambayo kwa sehemu kubwa ndiyo imekuwa ikisadia kulinda vyanzo vya maji.

Mratibu wa Programu ya Dodoma ya Kijani kutoka TFS, Alexander Mboya, alibainisha hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maagizo yaliyotolewa na Makamu wa Rais pamoja na jitihada zinazofanya na wakala huo kulinda mazingira nchini.

Mboya, alisema maagizo ambayo Makamu wa Rais aliyatoa Siku ya Mapinduzi ya Zanzibar Januri 12, mwaka huu wakati wa upandaji miti katika Shule ya Msingi Msalato jijini hapo, wameyapokea na wanakwenda kufanyia kazi.

Kadhalika, alisema kufanyia marekebisho utaratibu wa utoaji wa leseni za ukataji miti kwa ajili ya mkaa kutasaidia bidhaa za misitu nchini kuwa endelevu na kunufaisha wananchi bila kuathiri sekta nyingine.

Aidha, aliwataka wanchi kuendelea kulinda misitu ya asili kwa kuacha vitendo vya ukataji miti ovyo kwa ajili ya nishati ya mkaa na kuni.

"Pia wafugaji kuigiza mifugo yao kwenye misitu ya asili hili limekuwa changamoto kwetu TFS, kwani nakumbuka hata Rais wa Mstaafu Ali Hassan Mwinyi wakati wa utawala wake alishawahi kusema kuwa umaskini na uharibifu wa mazingira ni mapacha,"alisema Mboya.

Pia, alishauri uwepo wa mpango wa matumizi bora ya ardhi katika halmashauri zote nchini ili kuwepo kwa maeneo maalum kwa ajili ya malisho ya mifugo,hifadhi za misitu pamoja na vyanzo vya maji.

Akizungumzia majukumu ya wakala huo alisema moja ya kazi yao ni kuotesha miche ya miti na kuigawa kwa makundi mbalimbali kwa ajili ya kupanda kwenye makazi yao na maeneo ya taasisi.

"Mwaka jana tuliotesha miti zaidi ya miti milioni moja na kuigawa kwa watu mbalimbali kwa ajili ya kupanda katika maeneo yao lakini pia mwaka huu tumepanga kugawa idadi kama hiyo ya miti na hadi sasa tayari tumeotesha miti laki saba," alisema.

Hata hivyo, aliwataka watu wote ambao wamekuwa wakichukua miti katika kitalu cha TFS, kuhakikisha wanaitunza baada ya kuipanda ili ikuwe na kuonyesha thamani ya fedha iliyotumika.

Alisema: "Lengo siyo kupanda miti tuu bali kinachotakiwa ni kuhakikisha kuwa inatunzwa kwa kuimwagilia maji wakati ikiwa bado midogo na kuilinda dhidi ya mifugo".



Mkurugenzi wa Bonde la Mto Pangani Segule Segule (kulia) akiwaonyesha waandishi wa habari namna mto Muze ambao unatitirisha maji kwenda mto Zigi ikiwa ni ziara ya kufuatilia agizo la Waziri wa Maji, Jumaa Aweso alilotoa wiki iliyopita akiwa kwenye ziara Jijini Tanga. **PICHA: OSCAR ASSENGA**

# Watumishi wanaokaguliwa watakiwa kutoa ushirikiano

**Na Paul Mabeja,**DODOMA

NAIBU Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Ramadhani Kailima, amewataka watumishi wote wanaokaguliwa katika sekretarieti za mikoa na mamlaka za serikali za mitaa kutoa ushirikiano kwa vyombo vinavyofanya ukaguzi huo.

Kailima alibainisha hayo wakati akifunga mafunzo ya matumizi ya mfumo wa ukusanyaji wa mapato katika mamlaka za serikali za mitaa kwa wadau kutoka taasisi mbalimbali za serikali mkoani Dodoma.

Alisema kumezuka tabia ya baadhi ya watumishi kutokutoa ushirikiano kwa wakaguzi pindi wanapokuja kukagua baadhi ya miradi katika mamlaka za serikali za mitaa jambo hilo ni ukiukwaji wa sheria.

Kailima aliwasisitiza kuhakikisha wanafafanua hoja kila inapotokea katika muendelezo wa ukaguzi ili ziweze kupatiwa majibu kwa haraka na kupunguza hoja za wakaguzi na ikishindikana zipelekwe ngazi za juu kwa ajili ya kupatiwa majibu


Kadhalika, aliwashauri makatibu tawala wa mikoa kuhakikisha wanafanya vikao ili kuzichambua hoja zinazojitokeza kwa wakati na kupunguza hoja zinazojitokeza mara kwa mara.

Vilevile, alivitaka vyombo vyote vya ukaguzi kuhakikisha wanashirikiana na sekretarieti za mikoa ili kuweza kutatua kero zinazojitokeza wakati wakitekeleza majukumu yao.

Ofisa kutoka Mamlaka ya Serikali Mtandao, Mwanaisha Semboko, alisema mafunzo hayo yamekuwa na tija kwa taasisi zote za umma zinazoshirikiana na Ofisi ya Rais -TAMISEMI hasa katika suala la ukaguzi kwenye mifumo inayotumika kwenye ukusanyaji wa mapato.







Wafanyakazi wa Shirika la Umeme nchini (Tanesco) mkoa wa Mbeya wakiendelea na kazi ya kurejesha umeme katika Kata ya Uyole mwishoni mwa wiki baada ya kukatika kwa siku tatu kutokana na mafuriko yaliyotokea wiki iliyopita na kusababisha miundo mbinu mbalimbali kuharibika . **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wananchi wavamia msitu wa hifadhi, waanzisha mashamba

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BAADHI ya wananchi wa Kijiji cha Idugumbi wamevamia Msitu wa Hifadhi ya Safu za Mlima Mbeya, kuufyeka kwa lengo la kuanzisha mashamba jambo ambalo linahatarisha uwapo wa msitu huo pamoja na vyanzo vya maji vya mito mbalimbali.

Hali hiyo ilibainika juzi wakati maofisa wa Baraza la Taifa la Mazingira (NEMC) kutoka makao makuu na wa Wakala wa Huduma za Misitu nchini (TFS) walipofanya ziara ya kukagua hali ya mazingira katika safu za mlima huo.

Katika eneo hilo maofisa hao walishuhudia mashamba makubwa yakiwa yamelimwa ndani ya msitu huo huku yakiwa yamepandwa mazao ya aina mbalimbali.

Kutokana na hali hiyo NEMC ilitoa wiki mbili kwa maofisa wa TFS kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, kuwaondoa wananchi hao ndani ya msitu ili kulinda mazingira pamoja na vyanzo vya maji ambavyo vimeanza kupotea.

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samwel Gwamaka alisema hali aliyoiona inakatisha tamaa kutokana na mazingira ya msitu huo kuharibiwa kwa kiwango kikubwa.

Alisema ndani ya wiki mbili wananchi hao wanatakiwa waondolewe na wasijishughulishe te na na shughuli za kilimo pamoja na shughuli zingine zinazoharibu mazingira.

"Mtaangalia wenyewe mstakabali wa mazao ambayo yamepandwa, kama mtayafyeka ama la hilo mtajua wenyewe lakini ndani ya wiki mbili mnatakiwa muwe mmewaondoa watu wote hao na mshirikiane na Mkuu wa Wilaya," alisema Dk. Gwamaka.

Ofisa Misitu wa TFS Wilaya ya Mbeya, Danson Bashiri alisema walibaini uharibifu huo Oktoba mwaka jana walipofanya ziara na Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua na wakafanya mkutano na wananchi wa vijiji vinavyozunguka safu za mlima huo. Alisema walikubaliana kwamba wangewaondoa wakulima hao mapema kabla msimu wa kilimo haujaanza lakini ikashindikana baada ya Mkuu wa Wilaya kuwaeleza kwamba maaskari waliotakiwa kushiriki kwenye kazi hiyo walikuwa na majukumu mengine.

Alisema kwa sasa wanakusudia kwenda muda wowote kuwaondoa wakulima hao baada ya maaskari kumaliza majukumu yaliyokuwa yakiwakabili.

"Tulikuja hapa Oktoba 27 mwaka jana tukafanya mkutano na wananchi wa kijiji hiki cha Idugumbi, sasa kazi ya kuwaondoa imekwama kwa sababu ya majukumu yaliyokuwa yanawakabili maaskali," alisema Bashiri.

Alisema wakati mwingine huwa wanachelewa kubaini uharibifu wa misitu kwenye baadhi ya maeneo kutokana na ofisi yao kuwa na wafanyakazi wachache wa kufanya doria za mara kwa mara.

Meneja wa NEMC Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Glory Kombe alisema uharibifu wa mazingira unaofanywa na wananchi kwenye misitu hiyo unahatarisha maisha yao wenyewe kutokana na kuharibu vyanzo vya maji ambavyo wanavitumia.

Alisema maji yanayotoka kwenye misitu hiyo yanatumiwa na wananchi kwa ajili ya kunywa, shughuli za kilimo pamoja na kuzalisha nishati ya umeme.

Aliwataka wananchi wote wanaoishi jirani na misitu ya hifadhi kushiriki katika shughuli za uhifadhi badala ya kuwa sehemu ya waharibifu wa mazingira.

# DC apiga marufuku wanafunzi kufukuzwa kisa ukosefu mahitaji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI wilayani Mbeya imepiga marufuku wakuu wa shule za sekondari na walimu wakuu wa shule za msingi kuwafukuza wanafunzi wanaoanza darasa la kwanza na kidato cha kwanza kwa sababu ya kukosa baadhi ya mahitaji.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua alipiga marufuku hiyo mwishoni mwa wiki alipokuwa anagawa vishikwambi kwa walimu wakuu, wakuu wa shule na maofisa elimu kata wa Jiji la Mbeya.

Vishikwambi hivyo vimeandaliwa kwa ajili ya kuwasaidia viongozi hao kuandaa taarifa na kutunza kumbukumbu mbalimbali zinazohusu sekta ya elimu.

Alisema wanafunzi wote walioandikishwa kuanza masomo kwa mwaka huu wanatakiwa kuanza bila kuwekezwa vikwazo vya aina yoyote na walimu.

"Natoa maelekezo kwa shule zote za serikali, isitokee mtoto yeyote akarudishwa nyumbani kwa sababu ya kukosa vifaa, watoto wote wapokelewe hata kama wanavaa kandambili waendelee kusoma wakati vifaa vinatafutwa," alisema Dk. Chuachua.

Alisema kwa sasa serikali inaendelea na sera ya elimu bila malipo na hivyo walimu wanatakiwa kuzingatia jambo hilo na kufuata taratibu za kuanzisha michango ya aina yoyote ndani ya shule.

Aidha, aliwataka kutumia vishikwambi walivyokabidhiwa kwa ajili ya shughuli za elimu pekee na siyo vinginevyo huku akitahadharisha kuwachukulia hatua watakaovitumia kwa shughuli zingine.

Baadhi ya walimu waliokabidhiwa vishikwambi hivyo waliishukuru serikali kwa kuwapatia nyenzo hizo wakieleza kuwa zitawasaidia kufanya kazi kidijitali tofauti na ilivyokuwa awali ambapo walikuwa wanatumia nyenzo duni.

Ofisa Elimu wa Kata ya Mwasanga, Mwalimu Ambros Ngajilo alisema wakati mwingine walikuwa wanaandaa taarifa na kutunza kumbukumbu za elimu jambo ambalo lilikuwa linasababisha ufanisi kuwa mdogo. Alisema kioo cha simu ni kidogo kuliko cha kishikwambi na hivyo walikuwa wanatumia muda mrefu kuandaa taarifa na kusababisha kutozifikishwa kwa wakati mahali zinapohitajika. Ofisa Elimu wa Kata ya Isyesye, Mwalimu Gloria Nchelewa alisema vishikwambi hivyo vitawasaidia katika kuandaa taarifa za elimu katika maeneo yao ikiwemo uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la awali, darasa la kwanza na kidato cha kwanza.

Vilevile alisema vishikwambi hivyo watavitumia kwa ajili ya shughuli za kufundishia wanafunzi ikiwa ni pamoja na kuandaa masomo kwa kutumia vifaa hivyo. Mtakwimu wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Cosmas Kihovecho alisema waligawa vishikwambi 1,035 kwa maofisa wote wa Jiji hilo wanaohusika na sekta ya elimu.

# Halmashauri Mbeya zapigwa 'stop' kukopa fedha benki

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA.

SERIKALI mkoani Mbeya imezipiga marufuku halmashauri zote za mkoa huo kukopa fedha kwenye taasisi za fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa maelezo kuwa mikopo hiyo ndiyo chanzo cha ufisadi.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera alipiga marufuku hiyo wakati wa Kikao cha Kamati ya Ushauri ya mkoa huo (RCC) baada ya Halmashauri ya Wilaya ya Chunya kuomba kibali cha kukopa Sh. bilioni moja kwa ajili ya ujenzi wa Stendi ya Mabasi.

Homera alisema halmashauri zote zinatakiwa kutumia mapato ya ndani kutekeleza miradi badala ya kukopa, huku akikumbushia ufisadi uliofanyika baada ya Jiji la Mbeya kukopa fedha kwa ajili ya ujenzi wa Soko la Kimataifa la Mwanjelwa.

Alisema deni hilo linatakiwa kuwa somo kwa halmashauri zingine akieleza kuwa mpaka sasa bado halijalipwa licha ya jitihada mbalimbali ambazo zinafanywa na serikali kulipa pamoja na kuzungumza na benki ambayo fedha hizo zilikopwa.

Alisema Halmashauri ya Chunya ina uwezo wa kukusanya zaidi ya Sh. milioni 100 kila mwezi kutokana na sekta ya madini pekee, hivyo wanaweza wakawa wanatenga kiasi fulani cha fedha kila mwaka kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

"Marufuku kukopa fedha kutoka benki labda mimi siyo mkuu wa mkoa huu, hakuna halmashauri inayokopa sasa hivi, hapo mnasababisha watu wakajifungie chumbani wagawane fedha kama ilivyotokea hapa Jiji," alisema Homera.

Alisema fedha za kukopa zinakuwa na vikao vingi ambavyo vingine huwa vinafanyika kwa ajili ya watu kutengenezeana posho zisizokua na msingi wowote.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Simon Mayeka alisema wangepatiwa mkopo huo wangekuwa na uwezo wa kurejesha Sh. milioni 50 kila mwezi. Alisema waliamua kuomba mkopo huo ili kukamilisha ujenzi wa stendi hiyo tofauti na kutumia vyanzo vya ndani ambao alisema watatumia muda mrefu.

Hata hivyo aliahidi kuwa kutokana na katazo la Mkuu wa Mkoa, hawatakopa bali watadunduliza fedha zinazotokana na makusanyo ya ndani kukamilisha mradi huo.



Mpishi wa samaki ambae hajafahamika jina lake akikaanga samaki katika soko la samaki Bagamoyo mkoani Pwani, ambapo soko hilo linatumia nishati ya gesi kwa kukaanga samaki jambo ambalo linasadia kuhifadhi mazingira. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Yussuph Juma Mwenda ateuliwa Kamisha Mkuu ZRA

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS Dk. Hussein Ali Mwinyi amemteua Yussuph Juma Mwenda kuwa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA).

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Saada Mkuya Salum ndiye aliyetangaza uteuzi huo baada ya Dk. Mwinyi kumteua.

Hatua ya hiyo imekuja baada ya Serikali ya Zanzibar kuridhia mabadiliko ya Sheria Namba 11 ya mwaka 2022 ya kuazishwa kwa Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA)na kufuta Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB).

Akitoa taarifa kwa vyombo vya habari katika ofisi za mamlaka hiyo Mkuya alisema mchakato wa kuibadilisha bodi kwenda mamlaka umekamilika na kwamba sheria hiyo ilipitishwa rasmi Desemba 14 na Baraza la Wawakilishi na Desemba 29 Rais kuisaini na kutangazwa katika gazeti la serikali. Alisema pamoja na maendeleo mazuri ya ukusanyaji wa mapato chini ya ZRB serikali imeona ipo haja ya kukifanya chombo hicho sasa kuwa Mamlaka ya Ukusanyaji wa Mapato badala ya kuwa bodi. Hivyo aliwataka watendaji na wananchi kutoa ushirikiano mkubwa kwa mamlaka hiyo ili kufikia malengo katika ukusanyaji wa mapato nchini.

Alisema lengo kubwa la kutoka kwenye bodi kwenda kwenye mamlaka ni kujenga taasisi imara ambayo itaheshimika na kuleta mtazamo chanya wa kiutendaji.

Aidha, alisema sababu nyingine ni kuendana na mabadiliko makubwa ya kiutendaji na kimfumo katika taasisi za serikali kwa kuleta mabadiliko yatakayoendana na mahitaji ya nchi kama ilivyoelezwa na Sheria ya Utumishi wa Umma.

Mkuya alisema mabadiliko hayo yataleta tija kwa manufaa makubwa katika kuijenga taasisi imara ambayo itakuwa inaheshimika na kuleta mtazamo chanya kwa jamii.

Aliitaka mamlaka hiyo kuhakikisha mtu yeyote anaefanya makusudi kukwepa kodi kufuata sheria za usimamizi wa kodi zinafuatwa kikamilifu ili kodi kulipwa inavyostahili.

Kamishna Mkuu wa Mamlaka hiyo, Yussuph Mwenda, alimpongeza Rais Mwinyi kuendelea kuwa na imani kwake na watendaji wengine wa mamlaka hiyo na kuahidi kufanya kila linalowezekana ili kuhakikisha wanatimiza matarajio ya Wazanzibari. Alisema pia wanatarajia kuona mamlaka hiyo inakuwa chombo chenye weledi na kinatoa huduma bora kwa wafanyabiashara ambao ndiyo wadau wakubwa wa serikali.

Alisema tasisi hiyo haipo kwa ajili ya kuongeza kodi, kutumia nguvu kukusanya mapato bali ipo kushirikiana na walipa kodi ili kuona kila mfanyabiashara analipa kodi inayotakiwa.

Mwenda alisema kwa mujibu wa kifungu cha 38 cha Sheria ya Mamlaka hiyo kinaruhusu nyaraka, taarifa na nembo ambazo zilizopitishwa na ZRB kwa sasa ni nembo halali mpaka zitakapobadilishwa.

Hivyo aliwaomba wananchi kushirikiana na ZRA kuhakikisha wanapofanya manunuzi wanadai risiti na wafanyabiashara wanapofanya mauzo wanatoa risiti ili kuiwezesha serikali kupata mapato yake.

# Wajasiriamali watakiwa kushirikiana uendeshaji biashara

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Saidi Shaaban, amewataka wajasiriamali kushirikiana katika uendeshaji wa biashara zao ili kufikia kiwango chenye ubora kwa soko la utalii.

Aliyasema hayo jana visiwani hapa wakati akifungua mkutano wa siku maalumu ya bidhaa zinazozalishwa Zanzibar.

Alisema wajasiriamali wa Zanzibar ni wengi hivyo iko haja ya kushirikiana kwa pamoja kuunda jumuiya ya wafanyabiashara kutokana na bidhaa zinazofanana ili uzalishaji uwe bora na wenye kiwango cha matakwa ya mteja.

Alisema kuwa kuwapo na jumuiya ya wafanyabiashara za bidhaa mbalimbali ni rahisi kutambulika na kupata soko la ndani na nje ya nchi.

Hivyo aliwataka wajasiriamali kufahamu Mamlaka ya Uthibiti wa Leseni ( BRC ) ndiyo wenye uwezo wa kutoa leseni hivyo hakuna taasisi yoyote inayoruhusiwa kutoa leseni isipokuwa BRC.

Mwenyekiti wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar, Rahim Baluu, alisema kuwa wajasiriamali wa Zanzibar lazima wabadilike kutokana na hali ya sasa ya matumizi ya mitandao kuchukua nafasi kwa kuzitangaza bidhaa zao .

Alisema ipo haja kwa wajasiriamali wa Zanzibar kupewa elimu ya biashara ili kuwajengea uwezo pamoja na kuwa na utayari wa kuendesha biashara zao.

Hata hivyo aliwataka wajasiriamali hao kuweka alama ya ujumbe kwenye vifungashio wa kutunza mazingira ili baada ya matumizi visizagae ovyo.

# Zanzibar kuwa mwenyeji Mkutano wa Uwekezaji Afrika

**Na Mwandishi Wetu**

WAWEKEZAJI na wadau mbalimbali kutoka Afrika Mashariki na Kati wanatarajiwa kukutana Zanzibar kwa ajili ya mkutano wa kikanda kujadili uwekezaji endelevu.

Mkutano huo unaandaliwa na Kampuni ya MNCapita kutoka Afrika Kusini, ambayo inajihusisha na mawasiliano ya uwekezaji.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mkutano huo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya MNCapital, Michael Ndinisa, alisema mkutano huo wa mwaka 2023 utafanyika visiwani humo kwa siku mbili kuanzia Februari 22, mwaka huu.

Alisema kauli mbiu ya mkutano huo ni 'Kufikiria tena faida za uwekezaji katika kuwekeza kwa matokeo' kwamba utawaleta panoja wadau kujadili mambo mbalimbali yanayohusu uchangiaji wa maendeleo endelevu ya kiuchumi Afrika Mashariki na Kati kwa kuvutia uwekezaji mpya.

Alisema Tanzania imechaguliwa kuwa mwenyeji wa mkutano huu kwa kuwa imeendelea kuwa maarufu kama kitovu cha uwekezaji na imeonesha kukua na kuimarika kwa siasa na mazingira mazuri ya uwekezaji.

Ndinisa alisema baada ya janga la mlipuko wa ugonjwa wa corona serikali za mitaa na serikali kuu duniani zimekuwa zikiongeza juhudi katika kuinua uchumi wao na kupunguza athari zitokanazo na ugonjwa huo.

Alisema mkutano huu utatoa fursa kubwa kwa taasisi za uwekezaji kubaini fursa za uwekezaji na kufanikisha faida ya uwekezaji na kuleta matokeo kwa jamii.

Kwa mujibu wa Ndinisa ni ushahidi kuwa kazi iliyoko mbele itahitaji juhudi za pamoja kutoka kwa sekta ya umma na binafsi, hali ambayo inahitaji mabadiliko katika sera ili kurahisisha ufanyaji biashara, kuvutia ushiriki wa sekta binafsi mikakati ya kuinua uchumi.

"Ni muhimu sana kwa ajili ya kufanikisha ushirikiano wa sekta ya umma na binafsi kwa sekta hizi mbili za uchumi kufanya mikutano ya pamoja ya wadau ili kuwaleta pamoja kila mmoja katika maswala ya ushirikiano huo," alisema.

Alisema washiriki katika mkutano huo watakuwa na fursa ya kushirikisha wadau na kuchochea ushirikiano wa muda mrefu.

Alisema washiriki pia watakutana na wafanya maamuzi kutoka serikalini na sekta binafsi na wataalamu wa masuala ya uwekezaji.

# ‘Marufuku walimu kupigapicha wanafunzi kurusha mitandaoni’

**Na Thobias Mwanakatwe,** MKALAMA

MKUU wa Wilaya ya Mkalama, Sophia Kizigo, amewaonya walimu wilayani humo kutumia vishikwambi walivyokabidhiwa na serikali kwa kupiga picha wanafunzi na kuzituma kwenye mitandao ya kijamii.

Alitoa onyo hilo juzi wakati akikabidhi vishikwambi 706 kwa Maofisa Elimu, walimu wa shule za sekondari na msingi wilayani humo ili kurahisisha majukumu yao na kuleta mapinduzi chanya katika sekta hiyo kupandisha ufaulu kwa wanafunzi.

“Mmepokea vishikwambi hivi nendeni mkavitumie kujitajirisha nyie katika masuala ya elimu na msiende kupiga picha za wanafunzi na kuwaposti ‘Instagram’ na sehemu nyingine hiyo itakuwa kinyume na sheria na hatua kali zitachukuliwa dhidi yenu,” alisema.

Kizigo aliwataka kuvitunza na kutumia vishikwambi hivyo kupata maarifa mbalimbali ya kielimu na kuwa wabunifu katika kuongeza ufaulu kwa wanafunzi.

Pia, aliwataka walimu kuendelea kutekeleza majukumu yao ya kila siku na kuwahamasisha wazazi kupeleka wanafunzi kuripoti shule kwa kuwa tayari masomo yamekwishaanza.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, James Mkwega, aliwasisitiza walimu kutunza vishikwambi hivyo ili viweze kudumu kwa muda mrefu kwa kuwa ni moja ya njia ya mapinduzi ya kidijitali katika sekta ya hiyo.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, Asia Messos, aliishukuru serikali kwa kuleta vishikwambi hivyo ambayo ni ahadi iliyotolewa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kugawa vishikwambi katika wilaya zote nchini ili kutoa motisha kwa walimu katika kutekeleza majukumu yao.

Messos aliwaambia walimu hao kutambua kuwa vishikwambi hivyo ni mali ya serikali na kuhakikisha wanavitumia kwa lengo lililokusudiwa.



Ofisa Elimu Taaluma, Shule za Msingi wilaya ya Muheza Tanga, Beatus Mtumbuka akizungumza na walimu wa shule za msingi na sekondari juzi katika ukumbi wa mikutano ofisi ya udhibiti ubora wakati wa kikao cha kugawa vishkwambi kwa walimu ambapo zoezi hilo liliahirishwa mpaka hapo litakapopangwa tena. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## Wezi wa parachichi shambani kuchukuliwa hatua

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

SERIKALI mkoani Njombe imewataka wakulima kuwafichua wezi wa parachichi wanaoenda kwenye mashamba ya watu na kuiba.

Katibu Tawala Wilaya ya Njombe, Emmanuel George, akiongea kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, alitoa agizo hilo wakati wa mkutano wa wakulima uliofanyika mkoani hapa.

George alisema katika kukabiliana na wizi wa parachichi shambani ambao umekithiri mkoani humo, wakulima wanatakiwa kushirikiana na serikali kutoa taarifa itakayosaidia kuwakamata wahusika ili hatua kali za kisheria zichukuliwe dhidi yao.

Alisema wezi wa parachichi huwa wanaenda katika mashamba ya watu hasa nyakati za usiku na kuiba kisha kwenda kuyauza wakiwatumia madalali.

Alisema wakulima wamekuwa wakitumia muda, nguvu na gharama kubwa kutunza mashamba yao, lakini hakuna wanachonufaika kutokana na kuibiwa kwa matunda yao.

Alisema katika hatua za awali ambazo serikali ya mkoa huo imezichukua ni pamoja na kuwahoji watakaokuwa wanauza parachichi kwa wanunuzi ili kujiridhisha kama matunda hayo ni ya kwao.

“Sasa hivi ukienda kuuza parachichi utakutana na maswali tujue umetoa wapi na kama ni za kwako kuna shida kusema mimi ni mkulima wa Maheve nina shamba langu sehemu fulani,” alisema George.

Mkurugenzi wa asasi ya maendeleo ya wakulima Nyanda za Juu Kusini (NSHDA), Frank Msigwa, alisema pamoja na jitihada za kutafuta masoko nje ya nchi changamoto inayojitokeza kampuni zinazoingia mkataba na asasi hiyo hazipati parachichi kama walivyokubaliana.

“Hiyo imewahi kututokea hata msimu wa nyuma unakuta ushindani ukishaingia kwahiyo kuna kampuni ambazo tumeshaingia nazo mkataba hazipati ule mzigo kadri ya mkataba ambao tumekubaliana,” alisema Msigwa.

Wakulima wa parachichi mkoani humo, George Fute, Clementina Mwepelwa na Abel Mwinuka, walisema kukosekana kwa taarifa sahihi na kwa wakati za bei ya parachichi kunasababisha wakulima kuendelea kulanguliwa matunda yao.

“Kwanza wanunuzi wenyewe wawe na subira kwa kungoja matunda yakomae pia wawe waaminifu kwa kununua parachichi kwa bei nzuri,” alisema Clementina.

# Manyoni yaweka mikakati kuongeza ufaulu

**Na Thobias Mwanakatwe,** MANYONI

WILAYA ya Manyoni mkoani Singida, imeweka mikakati ya kuongeza ufaulu wa wanafunzi shule za msingi ikiwamo kuweka sheria ya kudhibiti utoro kwa wanafunzi.

Mikakati hiyo ilitangazwa juzi wakati wa kikao cha viongozi wa idara ya elimu msingi ambacho kilikuwa maalum kwa ajili ya kufanya tathmini ya matokeo ya darasa la saba 2022 na kuweka mikakati ya namna ya kuboresha ufundishaji ili kupandisha ufaulu.

Ofisa Elimu Msingi Halmashauri ya Manyoni, Hamisi Milowe, alisema matokeo ya mtihani wa taifa wa darasa saba mwaka jana hayakuwa mazuri ikilinganishwa na Mock ambayo yalitoa matumaini na mwelekeo wa kufanya vizuri zaidi.

“Lengo la serikali na kila shule iwe na ufaulu wa asilimia 85 hivyo msipofikia lengo hili mnashusha wastani wa ufaulu kwa halmashauri. Tuwe na mikakati mizuri ili tufikie lengo,” alisema.

Alisema ili kufikia malengo hayo watahiniwa wawe wanatumae vitabu vya mitihani (PIRA) ili kuongeza na kukuza uelewa na pia vyakula shuleni ili kupunguza watoto kukaa muda mrefu bila kula.

Alisema mkakati mwingine ni kuunda kamati ya taaluma ya kata ambayo wajumbe watakuwa ni walimu wakuu.

Kamati jukumu lake itakuwa ni kufatilia taaluma kwa shule zote ndani ya kata husika ambayo itakuwa inakutana kila Jumatatu kuona maendeleo ya shule.

Mkakati mwingine ni kuondoa utoro kwa kutoa motisha kwa wanafunzi na walimu wanaofanya vizuri shuleni, michezo, bendi na pia ziwapo sheria zitakazodhibiti utoro.

Aidha, Milowe aliwataka maofisa elimu kata na wakuu wa shule kusimamia miradi inayojengwa ilingane na thamani ya fedha zinazotolewa na serikali.

“Wakuu wa shule msikumbatie miradi shirikisheni walimu wote waijue ili inapotokea haupo kila mmoja aweze kuuelezea, kamati za usimamizi wa miradi ziundwe mapema,” alisema.

HABARI KIMATAIFA

# Watu 40 wafariki dunia kwa ajali ya ndege Nepal

**POKHARA,** NEPAL

MAOFISA wa mji wa Pokhara, wamesema takribani watu 40 wamefariki katika ajali ya ndege iliyoanguka karibu na uwanja wa ndege katikati mwa Nepal, ikiwa imebeba watu 72 ndani yake.

Kwa mujibu wa taarifa ya maofisa hao, ndege hiyo ni ya shirika la ndege la Yeti na ilikuwa inatoka Kathmandu kuelekea mji wa kitalii wa Pokhara, na kwamba ilianguka na kushika moto wakati ikitua.

Inabainishwa kuwa video zilizochapishwa kwenye mitandao ya kijamii zilionyesha ndege ikiruka chini chini kwenye eneo lenye watu wengi kabla ya kuzunguka kwa kasi.

Msemaji wa jeshi la Nepal alisema kulikuwa na abiria 68 ndani ya ndege hiyo, wakiwemo takribani raia 15 wa kigeni, 53 wanasemekana kuwa ni Wanepali na wafanyakazi wa ndege wanne.

Alieleza kuwa raia wa kigeni waliokuwepo kwenye ndege hiyo ni Wahindi watano, Warussia wanne, Wakorea wawili, mmoja kutoka Ireland, Australia, Argentina na Ufaransa.

"Mamia ya wanajeshi wa Nepal wanashiriki katika operesheni hiyo katika eneo la ajali kwenye korongo la Mto Seti, kilomita moja na nusu tu kutoka uwanja wa ndege," alisema na kuongeza:

"Video iliyochukuliwa wakati ndege hiyo ikishuka inaonyesha moshi mzito ukifuka na kuwaka vifusi, tunatarajia kupata miili zaidi, na ndege ilivunjika vipande vipande," alisema.

Waziri Mkuu, Pushpa Kamal Dahal aliitisha kikao cha dharura cha baraza lake la mawaziri na kuvitaka vyombo vya dola kufanyia kazi shughuli za uokoaji.

Inaelezwa kwamba ajali za ndege si za kawaida nchini Nepal, mara nyingi kutokana na njia zake za kukimbia zilizo mbali na mabadiliko ya ghafla ya hali ya hewa ambayo yanaweza kuleta hali ya hatari.

Ndege zingine zilizowahi kudondoka katika taifa hilo ni ya Tara Air ilianguka Mei 2022 katika wilaya ya kaskazini mwa Nepal ya Mustang, na kuua watu 22.

Pia mwanzoni mwa mwaka 2018, watu 51 walipoteza maisha wakati ndege ya US-Bangla iliyokuwa ikisafiri kutoka Dhaka nchini Bangladesh iliposhika moto ilipokuwa ikitua Kathmandu.

**BBC**



Wafanyakazi wa Idara ya Uokoaji Ukraine wakiwaokoa manusura baada ya kombora la Russia kudondosha upande wa ghorofa lililokuwa na watu ndani yake juzi. **PICHA: MTANDAO.**

# 12 wauawa shambulizi la Russia nchini Ukraine

**DNIPRO,** UKRAINE

Russia imeanzisha mashambulizi mapya ya makombora kote Ukraine, na kuuwa takriban watu 12 katika shambulizi kwenye jengo la ghorofa katika mji wa mashariki wa Dnipro.

Maofisa wa Ukraine walisema shambulio hilo baya lililotokea mwishoni mwa juma lililopita huko Dnipro liligonga lango la jengo la ghorofa tisa na kuzigeuza kuwa vifusi vinavyofuka moshi, na kusababisha majeruhi 73, wakiwemo watoto 14, na kwamba shambulio hilo linatajwa kuwa baya zaidi kuwahi kutokea katika miezi kadhaa.

Inaelezwa kuwa umati mkubwa wa watu ulikusanyika kutazama juhudi za uokoaji huku wengine wakiungana na wafanyakazi wa uokoaji katika shughuli za kuwatafuta manusura.

Maofisa walibainisha kuwa hadi kufikia jana, watu 37 waliokolewa kutoka kwenye jengo hilo, wakiwemo watoto sita, na kwamba miji mingine kadhaa, ikiwemo Kyiv, Kharkiv na Odesa, pia ilipigwa.

Hapo awali, Uingereza ilisema itatuma vifaru vya Challenger 2 nchini Ukraine kusaidia ulinzi wa nchi hiyo.

Waziri Mkuu wa Uingereza, Rishi Sunak, alisema kuwa Challengers, tanki kuu la vita la jeshi la Uingereza, litasaidia vikosi vya Kyiv kuwarudisha nyuma wanajeshi wa Russia.

Russia ilijibu kwa kusema kuwa kutoa silaha zaidi kwa Ukraine kutasababisha operesheni zake kuimarika na vifo zaidi vya raia.

Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, alisema mashambulizi ya Russia dhidi ya maeneo ya kiraia yanaweza kusitishwa ikiwa tu washirika wa Magharibi wa Ukraine watatoa silaha muhimu.

"Ni nini kinahitajika kwa hili? Silaha hizo ambazo ziko kwenye bohari za washirika wetu na ambazo askari wetu wanangojea sana," alisema.

Aliongeza kuwa vikosi vyake vilidungua zaidi ya makombora 20 kati ya 30 ya Russia. **BBC**

## Dhoruba yaendelea kuikumba California

**CALIFORNIA,** MAREKANI

TANGU mwishoni wa Desemba 2022 dhoruba kadhaa zimeuwa takriban watu 19, huku huduma za dharura za California nchini Marekani zikiamuru watu 6,000 kuondolewa, na kwamba mwishoni mwa juma janga hilo limesababisha zaidi ya watu wengine 20,000 kukosa huduma ya umeme.

Mkurugenzi wa ofisi ya Gavana wa California ya huduma ya dharura Nancy Ward, wakati akizungumza na waandishi wa habari jana, alisema athari za dhoruba hizo zimekuwa kubwa.

Alisema dhoruba zinaendelea kuwa hatari katika jumuiya kote California, akieleza kuwa tayari hadi sasa wameshuhudia dhoruba kubwa katika jimbo hilo ambazo zimesababisha uharibifu, na kwamba bado kuna nyingine zina tabiriwa kutokea.

"Kumekuwa na mafuriko, uharibifu wa nyumba huku majani ya miti yakitanda kwenye barabara na maporomoko ya matope. Kwa kuwa mvua kubwa tayari zimenyesha hali hiyo inaongeza ukubwa wa tatizo," alisema.

Hata hivyo hali ya mvua na kudondoka theruji kunatarajiwa kutasababisha hali kuwa mbaya zaidi, huku Ward akionya kwamba ni vyema wakazi wakachukua tahadhari zaidi.

Mtaalamu wa hali ya hewa David Lawrence, alisema katika siku 18 zilizopita jimbo hilo lililokumbwa na ukame limekuwa na mvua za wastani baada ya kupata mvua ya zaidi ya inchi tisa kwa siku kiasi ambacho kimesababisha baadhi ya maeneo kufikisha wastani wa mvua za kila mwaka. **VOA**

## Uingereza yamuwekea vikwazo mwendesha mashtaka Iran

**LONDON** UINGEREZA

UINGEREZA imemuwekea vikwazo mwendesha mashtaka mkuu wa Iran, Mohammad Jafar Montazeri kutokana na kunyongwa kwa aliyekuwa ofisa wa ngazi ya juu wa ulinzi wa Iran, mwenye uraia pacha wa Uingereza, Alireza Akbari kwa tuhuma za ujasusi.

Waziri wa Mambo ya Nje, James Cleverly, alisema vikwazo hivyo vinasisitiza kuchukizwa kwa Uingereza dhidi ya kunyongwa kwa Akbari, na kwamba mwendesha mashtaka mkuu ndiye kiini cha matumizi ya Iran ya hukumu ya kifo.

Aidha, Cleverly aliitaka serikali ya Iran kuwajibika kwa ukiukaji wa haki za binadamu.

Inaelezwa kuwa hukumu hiyo inaonekana kuweka shinikizo zaidi kwa Iran huku uhusiano wake na nchi za Magharibi ukizidi kuzorota tangu mazungumzo ya kufufua makubaliano ya nyuklia ya 2015 na Tehran ilipoanzisha ukandamizaji mkali dhidi ya waandamanaji mwaka jana. **DW**

# STRAIKA POLISI TZ KAMA SAIDO

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa Polisi Tanzania raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Enock Mayala, juzi alifunga mabao mawili, akiiwezesha timu hiyo kushinda ugenini, Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa mkoani Lindi, mabao 2-0 dhidi ya Namungo kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara akiingia katika orodha ya wachezaji waliosajiliwa kipindi cha dirisha dogo na kupachika mabao mechi yao ya kwanza tu.

Mayala ameingia kwenye rekodi aliyoiweka kiungo mshambuliaji wa Simba, Saido Ntibazonkiza, ambaye alicheza mechi ya kwanza akiwa amesajiliwa akitokea Geita Gold katika kipindi hiki cha dirisha dogo lililofungwa jana saa sita usiku, mechi yake ya kwanza tu akifunga mabao matatu 'hat-trick' na kuiwezesha timu yake kushinda mabao 7-1 dhidi ya Tanzania Prisons.

Hivi karibuni Makamu Mwenyekiti wa Polisi Tanzania, Robert Munisi, alisema pamoja na kumuachia straika Vitalis Mayanga, lakini wamesajili mastraika watatu ambao watakuwa na kazi ya kuiondoa mkiani, ambao ni Kelvin Sabato, Ibrahim Hilika na straika huyo ambaye tayari ameshaanza kufanya vitu vyake.

Kocha Msaidizi wa Polisi Tanzania, John Tamba, alisema ameonyesha kufurahishwa na straika huyo akisema atawasaidia sana kwani tatizo lao lilikuwa ni mtu wa kuweka mpira ndani ya wavu.

"Nimepokea kwa furaha kubwa, tulikuwa na uhaba wa mfungaji tunashukuru, mchezaji huyu tumefanya mazoezi wiki mbili, hakucheza mechi za nyuma kwa sababu hakuwa na vibali, kwa sasa vimekamilika sasa ndiyo ameanza, na bado tuna vita ya kujikwamua mkiani," alisema Tamba.

Kocha Mkuu wa Namungo, Denis Kitambi, alisema lawama zote atupiwe yeye kwa timu yake kukubali kipigo cha mabao 2-0 nyumbani.

"Timu kama haikucheza vizuri, lawama lazima abebe mwalimu, inasikitisha kufungwa na timu ya chini halafu iko pungufu, tumetengeneza nafasi ambazo hatukuweza kuzitumia, safu yangu ya ulinzi haikuwa nzuri, nitatumia muda uliopo kurekebisha hali, lakini mimi ndiyo nabeba lawama kwa hili," alisema kocha huyo.

Polisi Tanzania imefikisha pointi 14 kwa mechi 20 ilizocheza ikiwa nafasi ya 15, huku Namungo ikiwa nafasi ya sita kwa pointi 26.




Mshambuliaji wa Liverpool, Mahamed Salah, akijaribu kuinusuru timu yake kwa kipigo dhidi ya Brighton & Hove Albion, lakini kipa Robert Sanchez, akawa makini kulinda ushindi wao wa mabao 3-0, kwenye mechi hiyo ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Falmer juzi. **PICHA: MTANDAO**

# Mbuni yazinduka Championship

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kushindwa kupata ushindi kwa mechi kadhaa, timu ya Mbuni FC juzi iliibuka na ushindi mnono wa mabao 4-1 dhidi ya Mashujaa, mechi ya Ligi ya Championship iliyochezwa Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

Ushindi huo umewawezesha kufikisha pointi 21 na kuendelea kupigania nafasi ya kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao kwa kuingia moja kwa moja kwenye nafasi mbili za juu, au kucheza mechi za mchujo kama inashika nafasi ya tatu au ya nne.

Mabao ya washindi yalifungwa na Erickson Kabegi, Michael Mgimwa akipachika bao la pili, huku la tatu likiwekwa kwenye kamba na Jonathan Masimba, kabla ya Hassan Timbe kukamilisha kwa kufunga la nne.

Matokeo ya mechi zingine za Championship iliyochezwa juzi yalikuwa kwenye Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga, wenyeji African Sports wakizabuliwa mabao 2-0 dhidi ya Kitayoce, Fountain Gate ikaichapa Pamba bao 1-0 kwenye Uwanja wa CCM Gairo, Morogoro, Copco ikalazimishwa sare ya mabao 2-2 nyumbani Uwanja wa CCM Kirumba Mwanza dhidi ya Mbeya Kwanza, Transit Camp ikaidungua Ndanda bao 1-0, Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, na Biashara United ikiwa Uwanja wa Karume, Musoma mkoani Mara ilitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya KenGold.

Kwa matokeo hayo, Kitayoce imekwea kileleni ikiwa na pointi 35, ikiiacha JKT Tanzania ikiwa na pointi zake 24 ambapo ilitarajiwa kucheza dhidi ya Gwambina ambayo ni kama imejitoa au imesusa kucheza michuano hiyo kwani haijafika uwanjani kwenye mechi kadhaa.

Wakati huo huo, straika wa kikongomani Ngoi wa Ngoi Fabrice wa Kitayosce na Mtanzania Deogratius Kulwa wa Pamba wanaongoza kwenye orodha ya wafumania nyavu wakiwa na mabao saba kila mmoja.

Wachezaji hao wanafuatiwa na wachezaji wawili wa JKT Tanzania waliofunga mabao sita kila mmoja ambao ni Edward Songo na Martin Kisi, huku Emmanuel Steven wa KenGold na Adam Uledi wa Ndanda, kila mmoja akiwa amepachika mabao matano.

## Kampeni uchaguzi Simba zaanza rasmi

**Na Saada Akida**

MWENYEKITI wa Kamati ya Uchaguzi ya Klabu ya Simba, Boniface Lihamwike, ametangaza majina 14, yaliyopitishwa na kuruhusiwa kuanza rasmi kampeni kuanzia jana hadi Januari 28 kuelekea uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Januari 29, mwaka huu.

Wagombea waliopita katika nafasi ya Mwenyekiti ni wawili, ambao ni wakili Mosses Kiluwa na Murtaza Mangungu anayetetea nafasi yake ya uenyekiti baada ya kumaliza muda wake.

Wajumbe ni Seif Muba, Seleman Haroub, Idd Kitete, Issa Masoud, Abubakari Zebo, Abdallah Mgomba, Edward Mweladzi, Rashid Khamsini, Asha Baraka, Pendo Aidan, Rodney Karambo na Aziz Mohamed.

Akizungumza na gazeti hili jana, Lihamwike alisema baada ya kupitisha majina hayo wagombea wanatakiwa kuanza rasmi kampeni ambazo zitadumu hadi Januari 28 kabla ya uchaguzi huo kufanyika Januari 29, mwaka huu.

Aliwataka wagombea hao kufanya kampeni kwa kuzingatia katiba ya nchini na kanuni zinazowaongoza kwa sababu lengo ni kuona uchaguzi ukiwa wa haki na wazi ili kupata viongozi walio sahihi.

"Mchakato wa uchaguzi ulianza Novemba 26, mwaka jana kwa kupitia majina mbalimbali ikiwamo kufanya tathmini, pingamizi na wale waliokata rufaa katika Kamati ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), baada ya kujiridhisha, tunatamka majina hayo 14 rasmi wataanza kampeni za uchaguzi," alisema Mwenyekiti huyo.

## Zimamoto yataka ubingwa Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

LICHA ya kuzidiwa kwa alama 11 zaidi na vinara wa Ligi Kuu Zanzibar, Malindi FC walipo kileleni wakiwa na pointi 34, Kocha Mkuu wa timu ya Zimamoto, Mohmed Ali Hilali 'Tedy', amesema wanaanza mchezo wao wa mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Zanzibar kwa matarajio ya kuutafuta ubingwa wa ligi hiyo msimu huu.

Zimamoto FC itashuka dimbani leo kuwavaa Maafande wa Kipanga, mchezo utakaochezwa katika Dimba la Amaan majira ya saa kumi jioni.

Akizungumza na gazeti hili jana, kocha huyo alisema anajua katika mzunguko huu wa lala salama utakuwa mgumu, lakini amejipanga kupambana nao ili kuhakikisha lengo la kunyakuwa ubingwa huo msimu huu linatimia.

"Tumejipanga kuhakikisha tunapata alama tatu katika mchezo wetu huu, lakini mipango mikubwa ni kuhakikisha tunashinda mfululizo katika mzunguko huu wa pili ili lengo la kutwaa ubingwa msimu huu litimie," alisema. Timu ya Zimamoto ipo nafasi ya sita katika msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na alama 23 wakati kipanga ipo nafasi ya 10 ikiwa na alama 18.

Hata hivyo, juzi timu ya Polisi FC ilishindwa kutamba baada ya kutoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Dulla Boys mchezo uliochezwa Uwanja wa Amaan majira ya saa kumi za alasiri , wakati saa moja usiku timu ya Malindi ilifanikiwa kurejea kileleni kwa kufikisha alama 34 baada ya kuwafunga timu ya Black Sailor mabao 2-1 katika raundi ya 16 ya ligi hiyo.

## ZISIKUPITE

### MADUEKE ATAKIWA CHELSEA

CHELSEA wametenga dau la euro milioni 30 kumnunua winga wa PSV Eindhoven, Noni Madueke mwenye umri wa miaka 20. (***ESPN***)

### KEITA KUONDOKA LIVER

LIVERPOOL wamemaliza mazungumzo ya mkataba na kiungo wa kati, Naby Keita na watamruhusu mchezaji huyo wa kimataifa wa Guinea mwenye umri wa miaka 27, kuondoka kwa uhamisho wa bure msimu wa majira ya joto. (***Football Insider***)

### ANTONIO NA CHELSEA

CHELSEA walikuwa na ofa ya mkopo kwa mshambuliaji wa Jamaica, Michail Antonio, mwenye umri wa miaka 32, iliyokataliwa na West Ham. (***Guardian***)

### BARCA YAMTULIZA DEPAY

BARCELONA hawana haraka ya kumuuza mshambuliaji wa Uholanzi, Memphis Depay na wana furaha kumbakisha mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, hadi mkataba wake utakapokamilika msimu wa majira ya joto. (***Athletic***)

### ELANGA ATAKIWA EVERTON

KLABU ya Everton inataka kumsajili winga wa Uswisi, Anthony Elanga, mwenye umri wa miaka 20 kutoka Manchester United. (***Football Insider***)

### BISSAKA GHARAMA KUBWA

KLABU ya Crystal Palace inahofia gharama za kumsajili beki wa kulia, Aaron Wan-Bissaka mwenye umri wa miaka 25, kutoka Manchester United. (***Sun***)

### BELLINGHAM KIPAUMBELE

KLABU ya Real Madrid inamfanya kiungo wa kati wa England na Borussia Dortmund, Jude Bellingham mwenye umri wa miaka 19, kuwa kipaumbele katika soko la usajili. (***Fichajes***)

### PORRO SAFI SPORTING

KLABU ya Tottenham itakutana na Sporting Lisbon wiki hii kujadili kuhusu dili la beki wa kulia wa Hispania, Pedro Porro, mwenye umri wa miaka 23, ambaye amekubaliana masharti binafsi na klabu hiyo. (***Mirror***)

### SPURS YAMTAKA HINCAPIE

KLABU ya Tottenham Hotspur inapanga kumnunua beki wa Bayer Leverkusen na Ecuador, Piero Hincapie mwenye umri wa miaka 21 kwa pauni milioni 20. (***Sun***)

### WOLVES KUMNUNUA LASCELLES

KLABU ya Wolves ina nia ya kumnunua beki wa kati wa Newcastle, Jamaal Lascelles, mwenye umri wa miaka 29, ikiwa hawataweza kumsajili Craig Dawson (32), kutoka West Ham. (***Football Insider***)

### DANILO ATAKIWA FOREST

KLABU ya Nottingham Forest inakaribia kumsajili kiungo wa kati wa Palmeiras Mbrazili Danilo, 21. (***90min***).

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# KLOPP AIPONDA LIVERPOOL KUCHEZA VIBAYA BRIGHTON

**Nimechanganyikiwa sana, hongera washindi kwa mchezo bora, hatukuwa wazuri...**

**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, ameshutumu juhudi za timu yake katika kichapo cha aibu cha mabao 3-0 kwenye Ligi Kuu England ugenini kutoka kwa Brighton & Hove Albion ambacho alikiita kibaya zaidi kuwahi kutokea katika utawala wake.

**Winga Solly March alifunga mara mbili na kutengeneza la tatu kwa Brighton huku wakitawala mchezo kuanzia mwanzo hadi mwisho, na Liverpool wakishindwa kuunganisha hata shambulizi moja zuri.**

"Nimechanganyikiwa sana, hongera Brighton kwa mchezo bora. Hatukuwa wazuri leo (juzi)," alisema Klopp.

"Kufanya vizuri zaidi kuliko leo (juzi) kunapaswa kuwa rahisi, kwa sababu hii ni hatua ya chini sana. Siwezi kukumbuka mchezo huu mbaya zaidi," aliongeza.

Licha ya kufungwa 3-1 na Brentford katika mchezo wao wa mwisho wa Ligi Kuu England Januari 2, Klopp alisema kwamba alikuwa na uhakika akija kwenye mchezo wa Jumamosi kikosi chake kingeweza kupata ushindi unaohitajika sana.

"Hakukuwa na dalili ya kufanya vibaya kabla ya mchezo huu, lakini ndivyo inavyokuwa wakati mwingine. Hakuna kitu ambacho nilifikiria kwamba hii inaweza kutokea."

Msimu wa Liverpool umekatizwa na matokeo duni na majeraha kwa wachezaji muhimu, huku nahodha Virgil van Dijk akikosekana kwa sababu ya maumivu ya misuli ya paja na aliyesajiliwa hivi majuzi Cody Gakpo akianzia mbele kutokana na kukosekana kwa Darwin Nunez.

Kutokana na hali hiyo, 'Wekundu' hao walitatizika kumiliki mpira na Brighton waliweza kutumia vema nafasi walizopewa.

Liverpool wako katika nafasi ya nane kwenye msimamo wa ligi wakiwa na pointi 28, saba nyuma ya Newcastle United walio nafasi ya nne.

SportPesa
LIVE IN PLA

MECHI KALI
YOUNG AFRCANS
VERSUS
IHEFU FC
1 | 1.14
X | 6.26
2 | 17.61

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# ARSENAL YAMTAKA RAPHINHA WA BARCA



**LONDON,** England

VINARA wa Ligi Kuu England, Arsenal, wanaonekana kumkosa Mykhaylo Mudryk waliyekuwa wanamlenga kwa muda mrefu na sasa wanamtaka winga wa Barcelona, Raphinha.

'Washikabunduki' hao waliripotiwa kutuma maombi kadhaa kwa winga huyo wa Shakhtar Donetsk, lakini sasa anaonekana kujiunga na Chelsea baada ya kuanza mazungumzo ya ada na klabu hiyo ya Ukraine.

Kwa matokeo hayo, Arsenal watahitaji kuelekeza mawazo yao kwingine wakati wa dirisha hili la usajili la Januari ili kuimarisha kikosi chao.

Na sasa Arsenal wamemgeukia winga wa Barcelona Mbrazil Raphinha, kwa mujibu wa Sport Italia.

Winga huyo wa zamani wa Leeds United, alijiunga na Barcelona Julai kwa mkataba wa miaka mitano, lakini ameanza mechi 12 tu kati ya 22 akiwa na 'Blaugrana' hao.

Arsenal wanatumaini kuwa Raphinha atakuwa tayari kurejea England, kutokana na uzoefu wake wa awali kwenye ligi hiyo.

# *Guardiola: Man City haiwezi kushinda EPL*



**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amesema kwamba, Manchester City "haiwezi kushinda" taji la Ligi Kuu ya England, EPL, msimu huu.

City wamepitwa na vinara Arsenal kwa pointi tano baada ya kichapo cha mabao 2-1 kutoka kwa Manchester United kwenye mchezo wa dabi ya Manchester, Jumamosi.

Kupoteza huko kulifuatia City kuondolewa kwa Kombe la EFL na Southampton katikati ya wiki.

"Kitu cha mwisho ninachohofia ni mataji, mambo ya aina hii," alisema kabla ya kuikabili United, na Guardiola anaonekana kukubali kushindwa katika harakati za kushindana na Arsenal kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu.

"Sijali kuhusu Ligi Kuu na Kombe la Carabao," aliiambia BT Sport. "Hatuwezi kushinda. Tumeshinda sana, kwa hivyo si tatizo."

Lakini kocha huyo aliulizwa kuhusu maoni yake kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu msimu huu.

"Haya, bila shaka ninajali nani atashinda Ligi Kuu," alijibu. "Lakini hivi sasa, baada ya Southampton, ikiwa hatutashinda, hatushindi.

"Hatutashinda kila kitu miaka 25 ijayo, tunapambana, kwa sababu tuliona leo tutapigana na kucheza ili kushinda, lakini wakati mwingine mpira wa miguu ni hivyo.

"Tulipoteza Kombe la Carabao siku tatu zilizopita; tulipoteza. Lakini si juu ya kupoteza Kombe la Carabao, ni jinsi tunavyopoteza mchezo. Hii ndiyo sababu nilikuwa na huzuni, kwa kweli, huzuni.

"Ukweli ni kwamba ni ngumu kwa Manchester City kushinda taji la Ligi Kuu msimu huu, hali ni ngumu."

CHEZA USHINDE KASINO

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

# CHAMA AFUNGUKA, SIMBA YASHUSHA MKATA UMEME

**Adam Fungamwango na Hadija Mngwai**

WAKATI Klabu ya Simba ikimtangaza mchezaji wake mpya, Hemed Ismael Sawadogo raia wa Burkina Faso, kiungo mshambuliaji wa timu hiyo, Clatous Chama amesema amekuwa na 'assist' nyingi kwa sababu huwa hapendi kulazimisha kufunga hasa akiwa sehemu ambayo ni ngumu.

**Simba ambayo ipo kwenye ziara ya wiki moja Falme za Kiarabu na jana ikitoka sare ya mabao 2-2 katika mechi ya pili ya kirafiki dhidi ya CSKA Moscow ya Urusi, ilimtambulisha mchezaji huyo anayecheza nafasi ya kiungo mkabaji, nafasi ambayo ilikuwa ikilalamikiwa kwa muda mrefu na wanachama na mashabiki wa timu hiyo kuwa ina mapungufu.**

Klabu hiyo ilimtambulisha mchezaji huyo kwenye mitandao yake rasmi wa kijamii ambaye ametokea Klabu ya Difaa El Jadida ya Morocco aliyokuwa akiichezea mchezaji wa kimataifa wa Tanzania, Simon Msuva na jana aliwasili rasmi nchini akisubiri kuungana wenzake kesho.

Kabla ya timu hiyo, Sawadogo alikuwa akiichezea Ennpi ya Misri, akiwa pia amezichezea klabu mbalimbali kama RC Kadiogo, US Ouagadougou, AS Douanes na Salitas za nchini kwao Burkina Faso, Al Mabarra Club ya Lebanon na Al Arabi ya Kuwait.

Sawadogo anakuwa mchezaji wa pili kusajiliwa na klabu hiyo kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili baada ya Mrundi, Saidi Ntibazonkiza.

Wakati huo huo, kiungo mshambilaji wa timu hiyo Mzambia Chama amefunguka kuwa amekuwa akitoa pasi nyingi za mabao kwa sababu huwa hapendi kulazimisha kufunga sehemu ambayo hana uhakika kama atafanya hivyo.

Akizungumza akiwa Dubai juzi, Chama alisema anafunga akiwa na uhakika wa asimia kubwa kuwa atauweka mpira wavuni.

"Kuna watu wanasema mimi napenda ku 'assist' zaidi kuliko kufunga, hapana, mimi napenda vyote, kufunga na kutoa pasi za mwisho, lakini kubwa zaidi kuona timu inashinda, hata hivyo nakuwa na 'assist' nyingi kwa sababu sitaki kulazimisha, wakati mwingine unakuwa kwenye sehemu ambayo uko chini ya asilimia 40 za kufunga, lakini mwenzangu ana zaidi ya 60 au zaidi ya hapo, ninampa anafunga na wote tunafurahi," alisema Chama.

Akizungumzia kambi ya Dubai na mechi za kirafiki, alisema imewasaidia kuwajenga na wanachoangalia wao kwa sasa si kushinda mechi ili kupata mafunzo na kuingiza vitu vipya ambavyo vitawasaidia mbele ya safari.



Chama

## *Simba, CSKA Moscow zaonyeshana ukubwa*

INATOKA UK 32

ho Oliveira, aliwatoa Pape Sakho, Erasto Nyoni na Ntibazonkiza na kuwaingiza Mzamiru Yassin, Kibu Denis na Kyombo ambaye alibadili matokeo hayo kwa kufunga mara mbili.

Baada ya mechi hiyo, Simba imemaliza mechi zake za kirafiki na ilitarajiwa kuanza safari ya kurejea jijini Dar es Salaam, hiyo ikiwa ni baada ya Ijumaa iliyopita kucheza mchezo wake wa kwanza dhidi ya Al Dhafra ya Falme za Kiarabu na kufungwa bao 1-0.

Simba inayojiandaa na mechi za Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa Afrika, imemaliza mechi zake za kirafiki, ikiwa pia ni kambi fupi iliyoweka kwa muda wa wiki moja kutokana na mwaliko wa Rais wa Heshima wa klabu hiyo, Mohamed 'Mo' Dewji.

## Yanga, Ihefu FC mechi ya kisasi

INATOKA UK 32

leo saa 2:30 usiku ni Azam FC ikiwakaribisha Tanzania Prisons katika Dimba la Azam Complex uliopo Chamazi nje kidogo ya jiji la Dar es Salaam.

Kocha Msaidizi wa Azam FC, Aggrey Morris, alisema wamejiandaa vizuri kuwakabili Prisons na kuhakikisha wanapata matokeo mazuri.

"Tumefanyia kazi mapungufu yetu na wachezaji wamejiandaa vizuri na tuko tayari kwa ajili ya kusaka pointi tatu muhimu ili kujiweka katika nafasi tatu za juu katika msimamo," alisema.



## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMATATU - 16/01/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 3926 | Vitoria Setubal vs GD Fontinhas | 2.02 | 3.31 | 3.31 |
| 15:25 | 3614 | AL Riyadh vs AL Qaisoma | 1.98 | 3.11 | 3.65 |
| 15:30 | 5017 | Thailand vs Vietnam | 1.99 | 3.25 | 3.45 |
| 15:35 | 1512 | AL Khlood vs Al Orubah | 2.24 | 2.72 | 3.50 |
| 15:40 | 1412 | Al Jabalain vs AL Ain | 1.44 | 3.98 | 6.40 |
| 16:15 | 1816 | Iraq vs Qatar | 1.89 | 3.01 | 4.17 |
| 16:15 | 2911 | Kallithea FC vs Kalamata FC | 2.35 | 2.87 | 3.07 |
| 16:30 | 3315 | Hellas Verona Youth vs Empoli Youth | 2.55 | 3.50 | 2.55 |
| 18:00 | 1995 | Leon U20 vs Necaxa U20 | 1.87 | 3.70 | 3.75 |
| 18:00 | 2096 | Ethnikos Achnas vs Als Omonia | 1.64 | 3.50 | 4.86 |
| 18:30 | 2147 | Young Africans vs Ihefu FC | 1.14 | 6.26 | 17.61 |
| 19:00 | 1336 | Mamelodi Sundowns vs SuperSport Utd | 1.52 | 3.85 | 6.13 |
| 19:00 | 1948 | Mali vs Angola | 2.29 | 2.95 | 3.40 |
| 19:00 | 5355 | Zamalek vs Pyramids | 2.31 | 2.93 | 3.08 |
| 20:00 | 2383 | Omonia Nicosia vs AEL Limassol | 1.75 | 3.55 | 4.60 |
| 20:00 | 4843 | Doxa Katokopia vs Nea Salamis | 2.59 | 3.19 | 2.69 |
| 20:00 | 5464 | Pendikspor vs Erzurum BB | 1.87 | 3.40 | 3.70 |
| 20:15 | 1304 | Bahrain vs Oman | 2.53 | 2.77 | 2.91 |
| 20:30 | 2796 | Ionikos Nikea FC vs Volos | 2.69 | 3.24 | 2.54 |
| 20:30 | 5576 | Azam vs Tanzania Prisons | 1.37 | 4.14 | 7.32 |
| 20:45 | 5455 | Genoa vs Venezia | 1.67 | 3.58 | 4.97 |
| 21:00 | 2579 | Ingolstadt vs Erzgebirge Aue | 1.93 | 3.42 | 3.72 |
| 21:30 | 1998 | Beitar Jerusalem vs Maccabi Tel Aviv | 8.94 | 5.63 | 1.23 |
| 22:00 | 1050 | GD Estoril vs Casa Pia Atletico | 2.79 | 3.03 | 2.59 |
| 22:00 | 1158 | FC Oss vs Jong AZ Alkmaar | 3.16 | 3.65 | 2.02 |
| 22:00 | 2912 | Jong Utrecht vs Dordrecht | 1.84 | 3.69 | 3.69 |
| 22:00 | 3505 | FC Eindhoven vs Den Bosch | 1.54 | 4.04 | 5.33 |
| 22:00 | 4595 | Jong PSV vs VVV Venlo | 2.26 | 3.41 | 2.86 |
| 22:00 | 5204 | Crystal Palace U21 vs Fulham U23 | 2.58 | 3.60 | 2.30 |
| 22:30 | 3623 | Crotone vs Pescara Calcio | 2.21 | 3.19 | 3.29 |
| 22:45 | 1770 | Niort vs St Etienne | 3.12 | 3.27 | 2.20 |
| 22:45 | 3172 | Bradford PA vs Scarborough Athletic | 2.59 | 3.28 | 2.45 |
| 22:45 | 4851 | Empoli vs Sampdoria | 2.19 | 3.07 | 3.37 |
| 23:00 | 1589 | Port Vale vs Peterborough | 2.72 | 3.26 | 2.46 |
| 23:00 | 3428 | Bourg Peronnas vs Concarneau | 2.87 | 3.07 | 2.43 |
| 23:00 | 5021 | Cadiz CF vs Elche | 1.91 | 3.30 | 4.10 |
| 23:00 | 5329 | Albacete Balompie vs Leganes | 2.35 | 2.98 | 3.13 |

### JUMANNE - 17/01/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 00:15 | 1029 | Gil Vicente vs Vitoria Guimaraes | 2.38 | 3.18 | 2.94 |
| 01:00 | 5721 | Mount Pleasant FC vs Vere United FC | 1.34 | 4.09 | 8.96 |
| 01:30 | 1342 | Treze PB vs Auto Esporte Clube PB | 1.46 | 3.88 | 6.41 |
| 06:05 | 4854 | Club Leon vs Club Necaxa | 1.95 | 3.39 | 3.74 |
| 11:30 | 1675 | Sreenidi Deccan FC vs Minerva FC | 2.28 | 3.08 | 2.98 |
| 14:30 | 2773 | Sivasspor vs Bursa Niluferspor | 1.31 | 5.03 | 7.36 |
| 16:25 | 4687 | Al Rayyan SC vs AL Wakrah | 3.41 | 3.60 | 1.89 |
| 16:30 | 2212 | Rajasthan United vs Churchill Brothers | 2.29 | 3.12 | 2.92 |
| 17:30 | 5347 | Antalyaspor vs Kayserispor | 1.98 | 3.31 | 3.41 |
| 19:00 | 4857 | Al Sadd SC vs Lekhwiya SC | 2.15 | 3.74 | 2.72 |
| 19:00 | 5465 | Mozambique vs Libya | 3.91 | 2.95 | 2.10 |
| 20:00 | 2993 | Pafos FC vs Akritas Chlorakas | 1.13 | 6.79 | 15.53 |
| 20:30 | 2333 | Alanyaspor vs Galatasaray | 3.35 | 3.69 | 1.88 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumatatu Januari 16, 2023
Nipashe



Klopp aiponda Liverpool

UKURASA 21




Winga wa Simba, Pape Sakho, akipiga hesabu za kumtoka beki wa CSKA Moscow kwenye mechi ya kirafiki iliyopigwa Uwanja wa Sheikh Zayed jijini Abu Dhabi, Falme za Kiarabu na kumalizika kwa sare ya mabao 2-2 jana. **PICHA: SIMBA**

# Simba, CSKA Moscow zaonyeshana ukubwa

## ●●● Ntibazonkiza, Chama wampikia Kyombo akiipa sare, kasi na ufundi mwingi ukitawala...

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya Simba jana ilimaliza mechi zake za kirafiki Falme za Kiarabu kwa sare ya mabao 2-2 dhidi ya CSKA Moscow ya Urusi, kwenye mchezo mkali na wa kasi uliochezwa katika Uwanja wa Sheikh Zayed jijini Abu Dhabi.

**Simba ililazimika kutoka nyuma na kusawazisha mabao yote, baada ya kutanguliwa kufungwa 2-0 mpaka dakika ya 47.**

Habib Kyombo ndiye aliyefunga mabao yote mawili na kuiwezesha timu hiyo kupata sare dhidi ya miamba hiyo yenye rekodi ya kushiriki mara kwa mara michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na Europa League.

CSKA Moscow pia ni mabingwa wa Europa League msimu wa 2004/05, lakini pia ni mabingwa wa Ligi Kuu Urusi mara 13 na hadi sasa msimu huu wapo nafasi ya tano kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Katika mchezo wa jana, CSKA Moscow ilianza mechi kwa kasi na kufanikiwa kupata bao la kwanza dakika ya nne tu ya mchezo likifungwa na straika wao hatari raia wa Urusi, Fyodor Chalov baada ya kutokea piga nikupige kwenye lango la Simba.

Dakika moja baadaye, Warusi walipata penalti iliyotokana na straika huyo aliyefunga bao kuangushwa na Joash Onyango kwenye eneo la hatari.

Jesus Medina kiungo raia wa Paraguay, alichua jukumu la kupiga penalti hiyo, lakini alipaisha juu.

Hata hivyo, Medina alisawazisha makosa yake dakika ya 30 kwa kuweka mpira nyavuni na kuiandikia bao la pili timu yake, wakati akimalizia kazi safi iliyofanywa na Ivan Oblayakov.

Kipindi cha pili Simba ilianza kuonekana kufanya mashambulizi zaidi badala ya kuchezea sana mpira kati, na dakika tatu tu baada ya mapumziko, Kyombo aliuweka mpira wavuni.

Bao hilo lilitokana na gonga za hapa na pale zilizoonekana hazina madhara, lakini mpira ulipomfikia Saido Ntibazonkiza, alimwekea mfungaji aliyekuwa kwenye nafasi nzuri na aliitumia vizuri pasi hiyo na kuuweka pembeni, mpira ukagonga nguzo na kujaa wavuni.

Kyombo alifunga kwa mara nyingine tena bao, likiwa ni la kusawazisha kwa Simba katika dakika ya 75 baada ya kutumia vema pasi ya mwisho kutoka kwa Clatous Chama.

Katika mchezo huo, Kocha Robertin-

INAENDELEA UK 23

# Yanga, Ihefu FC mechi ya kisasi

**Na Saada Akida**

YANGA dhidi ya wababe wao wa Ligi Kuu Tanzani Bara, Ihefu FC, watashuka Uwanja wa Benjamin Mkapa leo, kila timu ikichukua tahadhari kutokana matokeo ya mzunguko wa kwanza kutoa nafasi kwa yeyote kushinda.

Katika mchezo huo wa Ligi Kuu Tanzania Bara raundi ya 20 utakaopigwa majira ya saa 12:30 jioni, Yanga itahitaji kulipa kisasi cha kufungwa mabao 2-1 na kuvunjwa rekodi yao ya kushinda mechi ya 49 mfululizo Novemba 28, mwaka jana katika Uwanja wa Highland Estates, Mbarali mkoani Mbeya, shukrani kwa Never Tigere na Lenny Kissu huku bao la Yanga likifungwa na Yanick Bangala.

Wakati Yanga ikitarajia kulipa kisasi hicho, itamkosa mfungaji wa bao lao pekee, Bangala pamoja na Stephane Aziz Ki, Bernard Morrison, Zawadi Mauya na Abdul Mshery ambaye amepata majeraha.

Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, amesema mechi itakuwa ya ushindani mkubwa na wanakutana na timu tofauti na ile waliyokutana nayo mzunguko wa kwanza.

Alisema Ihefu FC watakuwa na maingizo mapya na wamejiandaa vizuri zaidi yao, hivyo mchezo utakuwa mgumu na wanaenda kupambana kutafuta pointi tatu za mechi ya leo.

“Mazingira ya mechi ya mwanzo na sasa hivi ni tofauti kwa sababu tumejiandaa vizuri tutakuwa na kikosi bora na kuhakikisha tunafanya vizuri, hii ni mechi muhimu sana kwa sababu tunahitaji kupata matokeo ili kuendelea kuweka wigo mpana dhidi ya wanaotufukuzia katika msimamo wa ligi,” alisema Kaze.

Alisema Mudathiri Yahya hatakuwepo katika kikosi, kuhusu Kennedy Musonda, usajili mpya walihitaji kumuangalia katika mazoezi ya jana ili kuona uwezo wake.

Kocha Msaidizi wa Ihefu FC, Temmy Felix, alisema wamejiandaa vizuri kuhakikisha wanaenda kupata alama tatu ili kujiweka katika nafasi nzuri katika msimamo wa ligi hiyo.

“Tunasahau matokeo ya mechi ya kwanza, tunatambua Yanga itaingia kwa mfumo na mbinu tofauti na mchezo uliopita, tunahitaji kupata matokeo mazuri dhidi ya Yanga, ili kujiondoa katika presha ya kushuka daraja,” alisema Felix.

Mchezo mwingine utakaopigwa

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >